

KITENDAWILI

 Asanteni, ndugu zangu na dada zangu. Haya nayahesabu, kwa kweli, kwamba ni majaliwa makubwa kuwa hapa asubuhi ya leo, kuwazungumzia hawa watumishi wa Kristo, na wenzi wangu katika Injili, wafanyakazi wenzangu. Mimi si hodari wa kutoa hotuba; sina uwezo wa kufanya jambo hilo. Na ningetaka tu kuwakusanya wanaume pamoja, na wakati mwingine, namna hiyo, zaidi sana wale ambao wameninii, yale ambayo tungaliita ulimwenguni, wameshikilia, na kudhamini, mnaona, mmoja wa mikutano hii. Nami ningetaka kutoa sa—sababu ya Tumaini ninaloshindania, na kuwafanya ninyi ndugu mwone ya kwamba ni—ya kwamba si jambo lililojaa ninii—lililojaa ushirikina. Ni—ni Injili.

² Miaka mingi iliyopita, nilipofanya ziara yangu ya kwanza kwenda Phoenix, Arizona, ambako . . .

³ Nilikuwa tu nikifurahia kiamshakinywa changu, asubuhi ya leo, nikiwa pamoja na rafiki yangu wa kweli, Carl Williams, hapa pembeni. Nadhani nyote mnamfahamu Ndugu Carl Williams. Naomba msimame, Ndugu na Dada Williams. Yeye ni—yeye ni rais wa tawi la Wafanyibiashara wa Full Gospel huko Phoenix, Arizona, hasa, na Dada Williams, na kwa hiyo amethibitishwa kuwa rafiki yangu wa thamani sana.

⁴ Juma lililopita mkutanoni, na, ama juma moja kabla ya juma lililopita, huko Phoenix, nilikuwa nikisimulia juu ya wakati nilipofanya ziara yangu ya kwanza ya kwenda Phoenix. Nilikumbuka, wakati nilipokuwa mvulana mdogo, niliangalia na kusoma kila kitu nilichoweza, kwa sababu lilikuwa ni wazo langu, siku moja . . . Baba yangu alikuwa mpanda farasi, nami nilitaka kuwa kaoboi. Nilikuwa nimesoma magazeti fulani ya Kimagharibi, na kuona sinema nyingi mno, nikiwa mvulana mdogo. Na, kwa hiyo, nilikuwa nimemwona baba yangu akipanda farasi, nami nilifikiri hakika ningeweza kupanda farasi, pia, na shauku yangu ilikuwa ni kuja magharibi na—na kuwa mpanda farasi.

⁵ Nami nilikuwa nimesikia habari za Mlima wa Ushirikina. Bila shaka, Mholanzi Aliyepotea, ambalo ninaamini ni shimo Lililopotea la Mholanzi, jambo ambalo nafikiri ni hekaya ya uongo.

⁶ Na watu wengi sana sasa wananinii, kule nchini kwetu, inafikia ni wakati wa mashindano ya kaoboi, na kila mtu anavaa jinzi za bluu, lile kofia kubwa. Wanajaribu kuishi katika wakati u—uliopita. Wanaishi kitu fulani kilichopitwa na wakati. Nami ninashangaa ni kwa nini wanafanya hivyo. Kuna kitu ndani yao kuwafanya wafanye hivyo.

⁷ Lakini, unaona, nafikiri hiyo ndiyo shida ya mwenendo wetu wa Kikristo, leo. Tunajaribu kuishi katika wakati uliopita, kile mtu mwingine alichosema katika wakati mwingine. Na hilo halitafaa kitu wakati huu. Lakini ni jambo la ajabu ya kwamba watu wanapenda wazo fulani la mtindo wa kale, dansi fulani la zamani la mashambani, ama kaoboi fulani, kitu fulani, ama chochote kama hicho. Na hicho kitu kilicho halisi ndani yao, kinachowafanya kutaka kurudi huko nyuma, ni Injili. Wanataka Injili mpya iliyopambwa, kitu fulani cha kulingana na siku hii, mambo fulani makuu ya kulisimua hapa, na utamaduni mzuri na elimu. Bali hawataki Injili ya mtindo wa kale, ambapo kile kitu halisi ndani yao kinachowafanya watake kurudi huko nyuma. Huko ndiko kinapaswa kwenda, kurudi kwenye Hiyo. Lakini badala yake, wanarudi kwenye—kwenye kitu kingine. Ndipo wakati kitu fulani kinapoonyeshwa kutoka kwa Mungu, kinashangaza sana, si cha kawaida kwao, na wala hakilingani na maadili yao, na—na hawataki kukikubali.

⁸ Hakuna mtu angewaheshimu tena akina John Wesley, Sankey, Moody, Finney, au Finney, Knox, Calvin, yeyote wa watu hao, kuliko yeyote wetu sisi wahudumu ambao wanawathamini watu wa Mungu, heshima ambayo wangekuwa nayo kwa watu hao. Lakini, unaona, tunapanda juu. Hatuko katika wakati huo. Kila mmoja wa hao alitumikia wakati tofauti na katika kiwango tofauti. Tunamtumikia Mungu leo katika kiwango tofauti na vile walivyomtumikia. Kama kuna kesho, kutakuwa na kipindi, kutakuwa na Injili kwa ajili ya kipindi hicho, ambayo bado itaendelea mpaka jambo hilo lote likamilishwe katika Mungu, na Mungu anakuwa mmoja pamoja nasi.

⁹ Sasa, ninakumbuka asubuhi niliyochukua tochi, nisingesubiri kuuona ule Mlima wa Ushirikina. Ilinibidi kupanda kule juu. Lakini maskini tochi yangu ndogo haikufaa kitu. Nisingeweza kuona chochote. Vile vivuli vya kutisha vya kimizuka, na watu ambao wamekufa kwenye mlima huo, wakitafuta dhahabu, na u—unashikilia hadithi nyingi za ushirikina, kwa kweli. Na nilipojaribu na tochi yangu ndogo, kuangalia kote kote, ni—nisingeweza, nisingeweza kuona kitu chochote, na kila kitu kilikuwa ni cha kutisha. Mnajua nilichofanya? Niliketi tu kimya mpaka jua lilipochomoza. Wakati hilo jua, ambalo ni mfalme wa kila nuru, wakati lilipochomoza, tochi yangu ndogo haikufaa kitu, bali mizuka yote iliondoka. Niliona Mlima wa Ushirikina haukuwa na mizuka. Nilikuwa tayari kutembea niuingilie, nikauvumbue mwenyewe, kwa ile nuru kuu, jua, ambalo ni Neno la Mungu lililolenwa. Mungu alisema, “Na iwe nuru.” Na hilo ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Na lilipoangaza, mizuka yote ikatoweka.

¹⁰ Nami ninafikiri hivyo ndivyo ilivyo leo, ambapo nimeeleweka vibaya sana miongoni mwa ndugu, natamani ile

Nuru kuu, mfalme Nuru... Hakuna nuru nyingine. Hakuna yoyote ya nuru zetu za kujitengenezea itakayomulika kule leo. Haidhuru tutajenga viwanja vingapi vya michezo, huwezi kuona kitu, inakubidi kuchunguza jambo bayana uweze kabisa kuona nuru yoyote ile. Jua hili huzima zote, kwa maana ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Nami nafikiri, wakati Neno la Mungu lililodhihirishwa linapochomozea kwenye ushirikina wetu wote, unafifia. Unaona? Tunataka kujua Ukweli, kwamba tunaishi katika saa gani.

¹¹ Na, ndugu, tunaketi hapa, asubuhi ya leo, tukiwa madhehebu mengi mbalimbali, tukiwakilisha madhehebu mbalimbali. Sidhani hilo lina umuhimu.

¹² Nilikuwa nikichunga ng'ombe, huko Colorado. Ninakumbuka wakati mmoja wakati ambapo ningeninii... tungefanya msako, katika majira ya Kuchipua, kuwapeleka ng'ombe katika Msitu wa Arapajo. Nimeketi kule, kwa siku nyingi, huku mguu wangu umening'inizwa juu ya pembe ya matandiko, na kumwangelia mwangelizi wakati akihesabu hao ng'ombe wakipitia kwenye ua wa pepe, kutoka kwenye mali ya mtu binafsi, kuingia msituni.

¹³ Kila ranchi, ili kuingiza ng'ombe mle, inapaswa mtu kuwa na ninii, inapaswa kutoa tumba la nyasi kavu, naamini... si tumba la nyasi kavu, tani ya nyasi kavu, nafikiri ni tani mbili, kwa ng'ombe mmoja, inategemea ni kiasi gani Chama cha Wafanya Biashara kitakuruhusu kuingia mle nacho, chapa yako. Kwa sababu, kwa chapa hii na katika ranchi hii hutolewa kiasi fulani cha nyasi kavu, ndipo unaweza kuweka ng'ombe akale nyasi huko msituni. Ili kwamba msitu usijae ng'ombe, basi, na kiasi cha kutosha tu kuwatunza. Maana, kila mtu angekuwa anaingia. Na niliona... Ilikuwa ni Shirika la Hereford, ambalo hulisha kwenye msitu huo, katika sehemu yake hiyo, Msitu wa Arapajo. Nami nilimwangelia huyo mwangelizi.

¹⁴ Sasa, sisi, wetu walikuwa ni wale waitwao mshindi wa kutembea wa zamani, Mburuzo wa Mshindi. Migutatu ilikuwa papo hapo juu yetu. Bw. Grimes alikuwa amewajiri watu kumi na tano hivi, alikuwa na mamia kadhaa ya ng'ombe. Nasi tulikuwa na ng'ombe wachache pale, kampuni niliyokuwa nikifanyia kazi, ng'ombe mia nne ama mia tano. Lakini Grimes walifikia labda elfu moja mia tano, elfu moja mia nane, ilikuwa ni mche, Mche wa Almasi.

¹⁵ Nami nilimwangelia huyo mwangelizi. Inambidi kusimama pale na kuhesabu hao ng'ombe walipokuwa wakipita. Unajua, hakujali walikuwa wamebandikwa chapa gani. Kulikuwa na kitu kimoja alichochunguza, kilikuwa ni kishikizo cha damu kwenye sikio, kwa maana walipaswa kuwa ni Hereford waliosajiliwa kabla hawajaweza kula. Hiyo ni kwa sababu ya kuhifadhi ukoosafu wako. Unaona, ng'ombe wako anapaswa

awe amezalishwa, ndama wako hana budi kutoka kwenye dume ukoosafu. Na kwa hiyo, baada ya ng'ombe wengi sana, huna budi kuwa na ndume. Na wote wamechanganywa pamoja. Wote wanapaswa kuwa ni ng'ombe wa ukoosafu uliosajiliwa, asili bora. Unaweka ninii wako—wako—wako...mtiririko wako wa damu ukitiririka vizuri, basi, wa Shirika la Hereford.

¹⁶ Niliwazia, mara nyingi, “Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye ile Hukumu. Yeye hataona tunavaa chapa gani, bali ataangalia hicho kishikizo cha Damu, Yesu Kristo.” Hiyo itafanya kazi.

¹⁷ Kama tungejaribu kujifanya sisi sote, asubuhi ya leo, Waassemblies of God, tusingeweza kufanya hivyo. Tunajaribu kuwafanya Utakatifu wa Kipentekoste; tusingeweza kamwe kufanya hivyo. Tukijaribu kuwafanya Muungano wa Mekanisa; kamwe hatutaweza kufanya hivyo.

¹⁸ Bali kuna mahali pamoja tunapoweza kukutana, sisi sote, kama waaminio, chini ya Damu ya Yesu Kristo. Na hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu alipata kukutana na mwanadamu, ama atakapokutana daima na mwanadamu, ni chini ya Damu ya Yesu Kristo. Hapo ndipo tunapokuwa na vitu shirika.

¹⁹ Hivi majuzi, nilikuwa nikisoma mahali ambapo vijana mke na mume walikuwa wakitengana na lilikuwa ni jambo la kusikitisha. Wao, walikuwa wameishi pamoja kwa miaka kadhaa. Na kutokuelewana kukazuka kati yao, na maskini mama huyo, bibi na mumewe, walikuwa wakitaka kutengana. Nao walikuwa...Hakimu alikuwa ni rafiki yao. Akasema, “Sasa, kabla ya yote, inatupasa kumpeleka mtu kule na akauze vitu hivi, na kuchukua vile mlivyo navyo. Kama mtatalikiana, basi gawaneni tu mali mliyo nayo miongoni mwenu.” Wakasema watafanya hivyo.

²⁰ Wakaingia kwenye chumba cha kupokea wageni; wakagombana, wakapigana, na chochote kile, juu ya vitu vilivyokuwa katika chumba hicho. Wakaingia sebuleni, nao—nao wakafanya jambo lile lile pale, na chumba cha kulia, na jikoni. Hatimaye wakakumbuka, huko juu darini, ya kwamba walikuwa na vitu walivyokuwa wameweka kule. Kwa hiyo wote wawili wakapanda kwenda katika “upenu,” nadhani ndivyo mnavyoita hapa; mashariki, tunakuita, huko juu “darini.” Kwa hiyo wakapanda juu kule na wakatoa kasha la zamani. Nao walikuwa na nguo na kadhalika, kwamba, kwa hiyo walikuwa wakizichukua, na kugombana juu ya *hiki* na *kile*.

²¹ Na punde si punde, wakati walipoinua kitu fulani, wote wawili walikishika, na mikono yao ikashikana waliponyakua. Ilikuwa ni jozi ndogo ya viatu vyeupe. Ilikuwa ni ya m—mtoto mchanga waliyekuwa wamejaliwa kwenye ndoa yao, bali alikuwa ameaga dunia. Hapo, huku wameshikana mikono, mmoja asingeweza kusema, “ni vyangu,” huyo mwingine

asingeweza kusema, “ni vyangu.” Ilikuwa ni kitu walichokuwa nacho shirika. Kwa dakika chache tu, waliangaliana mmoja kwa mwingine. Mmoja asingeweza kuidai, wala huyo mwingine asingeweza kuidai. Kwa hiyo, walikuwa wamekumbatiana, na talaka ikabatilishwa.

²² Ninataka kuona jambo hilo, sisi Wabaptisti, na sisi Wamethodisti, na sisi Waassemblies, na Kanisa la Mungu, na chochote tungeweza kuwa. Huenda tukatofautiana kabisa kwa mambo, na kila kitu namna hiyo, hizo ni desturi zetu wenyewe zilizotuingiza katika jambo hilo. Bali kuna jambo moja tulilo nalo shirika, ndugu; Kristo, Yeye ni Neno. Hilo ndilo kusudi la sisi kuwa hapa; si kuzungumza juu ya tofauti zetu, bali ni kuzungumza juu ya yale tuliyo nayo shirika, Yesu Kristo.

Sasa na tuombe.

²³ Baba wa Mbinguni, Wewe ni Baba yetu, tunakushukuru, kwa sababu kwamba leo tuna matumaini ya Uzima wa Milele, kupitia kufufuka kutakatifu kwa Yesu Kristo. Tunaona Nuru za jioni zikiwaka. Mti uliosazwa na tunutu, umeliwa na madumadu; uliosazwa na madumadu; nzige wameula; nasi tunatambua ya kwamba wadudu hawa ni mdudu yule yule, akiwa tu kwenye hatua nyingine ya maisha yake. Nasi tunatambua ya kwamba tofauti za kanisa zingali ni mdudu yule yule wa Kirumi aliyeanza huko Nikea. Na kinachosazwa na mmoja, huyo mwingine anakila. Na inaonekana, kana kwamba, leo, kwamba tuko katika machafuko kama haya, na sasa tunaingia katika ile—ile halmashauri kuu, Baraza la Ekumeni la Makanisa, inaonekana kana kwamba kusingekuwa na chochote kilichosalia, matumaini yamekwisha.

²⁴ Lakini, kumbukeni, Neno la Mungu lisilokosea, kama vile jua lilivyochomoza kuonyesha wazi ushirikina, vivyo hivyo Wewe umeahidi, “Nitarudisha,” asema Bwana, “miaka yote iliyoharibiwa na madumadu, na tunutu, na kadhalika.” Jinsi ambavyo itarudishwa tena, na mti huo utaishi tena! Tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utashusha neema, na nguvu za kufufuka za Kristo, upate kurudisha, kutufufua sisi katika imani iliyo hai katika Neno lililo hai la siku hii. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

²⁵ Kidogo nimepwelewa na sauti, ndugu. Na kwa kuwa mimi si mnenaji, bali ni wakati tu wa kukusanyika pamoja, ili kwamba mtaona ninalomaanisha, nipo hapa. Kama mkinikamata nikifanya jambo lolote nje ya Neno hili na yale yaliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii, mnawiwa kuja kwangu, mnawiwa kuja kwangu mniambie. Lakini kama ninavyosema, kuna jambo moja tunaloweza kukubaliana, ni Kristo. Jambo hilo tunalishiriki sote pamoja. Yeye alitufia sisi sote. Tuko chini ya hiyo Damu.

²⁶ Sasa, siko hapa kufanya jambo lolote bali ni kujaribu kumsaidia kila mmoja wenu ninyi watu, ili kwamba jumuiya

hii itakuwa ni mahali bora zaidi baada ya ufufuo huu, kwa kuwa tumekutanika kwa ajili ya kusudi hili. Tumekutanika pamoja kwa ajili ya kusudi hili, ku—kufahamiana sisi kwa sisi, kufahamiana vizuri zaidi, kuwa na ushirika mmoja kwa mwingine. Hiyo ndiyo sababu mimi niko hapa asubuhi ya leo, hilo ndilo kusudi letu la kuwa na mkutano huu hapa, tupate kufahamiana.

²⁷ Sasa, tunatambua ya kwamba daima nyakati zote imekuwa hivyo. Hebu ngoja jambo dogo la ajabu sana lifanyike, ama jambo fulani tofauti, una kundi la waigaji wa kimwili wanaolifuata, ndipo una kila namna ya ushirikina. Na inapaswa tu kuwa namna hiyo. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Na mambo yanasemwa, kuhusu jambo Hilo, ambayo si ya kweli. Tunajua hivyo ndivyo imekuwa daima.

²⁸ Yesu alidhaniwa kuwa ni mwana haramu. Hakuwa. Yeye alikuwa vile hasa Biblia ilivyosema. Hao watu waliomwita hivyo... Yeye alikuwa ni dhahirisho la Neno la Mungu, lililodhahirishwa wazi.

²⁹ Na unaona, walisema, “Wanafunzi Wake walikuja wakauiba mwili Wake wakaenda zao, wakawahonga askari wa Kirumi.” Wangali wanaamini jambo hilo. Bali tunaamini na kujua, kwa Uwepe wake ulio hai sasa, ya kwamba alifufuka katika wafu, Naye yupo hapa pamoja nasi sasa. Tuna hakika na tunajua hivyo. Kila neno alilonena, na kuliahidi katika nyakati zote, limetimizwa, kama utaangalia jambo hilo. Hakuna kitu kingeweza kutimiza hilo, ila Mungu pekee. Sisi ni watumishi Wake.

³⁰ Na sasa niliwaza, asubuhi ya leo, ya kwamba ningesoma tu kifungu kifupi kutoka kwenye Maandiko, na kuzungumza na ninyi ndugu na dada hapa, ili tupate kuwa tu na mkutano mdogo wa pamoja.

³¹ Upepo huo hapo juu unanisumbua. Mimi... Hapa, hapa, hivyo ni sawa, sasa hivi uache tu, Ndugu Roy, kwa kuwa nitakaa tu kwa dakika chache.

³² Miaka michache iliyopita, yapata miaka kumi na tano iliyopita, nilikuwa nikiwinda na mtu aliyekuwa kinyozi, na pia alikuwa ni tabibu wa vitengele vya mguu, hiyo ni kusema, kukata sugu kutoka miguuni. Unajua, katika nyakati hizo mambo yalikuwa ni magumu, hakukuwa na pesa. Na huyu kinyozi rafiki yangu, nilikuwa nikichana nywele zangu na nilikuwa na... Alikuwa akinyoa nywele zangu, hasa, na alikuwa na mba mgongoni. Akasema, “Billy,” kasema, “inakupasa kuninii... itanibidi kukupa shampuu kidogo,” kasema, “una mba mwingi sana kwenye koti lako.”

Nami nikasema, “Vema, Jimmy.”

³³ Naye alikuwa akizungumza juu ya kuwinda koni, ndipo akachukua nyuma yake... mimi nilikuwa mchungaji wake, yeye

alifundisha Shule ya Jumapili; alikuwa ni mtu mzuri. Kuchukua yale aliyodhani kwamba ni hii Shampuu ya Lucky Tiger, kuimimina kichwani mwangu, kumbe ilikuwa ni asidi kaboliki.

³⁴ Ndipo ni—nikavaa kofia ya stokingi mimbarani mwangu, kwa majuma kadhaa. Leo, hiyo ingali inanisumbua, unaona, ile ninii tu kidogo. . . Unaona, ngozi yangu ya kichwa ingali ni nyororo, unaona.

³⁵ Na, hakuna, hiyo—hiyo—hiyo ni sawa sasa, kwa maana ilikuwa ni ule usiku wa mwisho, nami ninazibwa pumzi tu.

³⁶ Mke wangu alininunulia wigi ya kuvaa. Nisingevaa kofia mimbarani, ni kukosa heshima mbele za Kristo. Kama ukivaa kofia ndogo, wanasema, “Unataka kuwa askofu.” Na ni shida tupu. Alininunulia hiyo, bali kamwe sijapata ujasiri wa kuivaa. Laiti ningalikuwa na huo ujasiri, bali si—sina. Lakini ninahofu ingeonyesha kitu fulani, na, unajua. Na—na itanibidi tu kuliachia tu liende hivyo, nadhani.

³⁷ Na sasa ninataka tu kusoma Maandiko machache. Ambapo, Neno la Mungu halishindwi kamwe; langu litashindwa. Bali ninawataka mkumbuke jambo hili, ya kwamba katika kila kizazi ambacho. . .

³⁸ “Mungu, hapo mwanzo, ni Neno.” Daima alikuwa Neno. Na *Neno* ni “wazo lililotamkwa.” Unaona? Sasa, katika mawazo Yake, kile Yeye alichokuwa nacho, mpango wote, akijua mwisho kutoka mwanzo, Yeye ameyatamka tu katika Maneno, na Maneno hayo yamedhihirishwa.

³⁹ Ni kama tu jua, hilo ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Yeye alisema, “Na iwe nuru,” na ikawa nuru.

⁴⁰ Na kuna wakati wa utenganisho. Kulikuwa na wakati ambapo Mungu alitenganisha nuru na giza. Yeye daima hufanya hivyo. Kulikuwa na wakati ambapo alitenga ardhi na nchi, ama maji. Kuna utenga-. . . Alimtenganisha Paulo na Barnaba. Alimtenga Musa akamtoa Misri. Unaona, Yeye daima ni utenganisho. Na kuna nyakati zinakuja. Watu, watu wanaochukua huduma hizi, hawataki kufanya hivyo, bali ni lazima zifanyike. Unaona? Kuna wakati ambapo wale wanafunzi ilibidi wajitenge na watu wao wenyewe.

⁴¹ Paulo aliwageukia Mataifa, akaachana na Wayahudi, urithi wa Mungu. Wakati ulikuja ambapo ilimbidi kufanya jambo hilo. Walimsema; bali alitoa lile neno maarufu sana, “Sikuasi lile ono la Mbinguni.”

⁴² Na hebu niseme jambo lile lile, ndugu, unaona, ono la leo hii, unaona, ono la ahadi ya leo hii, Roho Mtakatifu n—nchini leo. Mungu aliahidi ya kwamba katika siku hii Yeye angemwaga Roho Mtakatifu juu yetu. Sasa, mimi nimepita nchini, huku na huko. Kumekuwa na ishara za ajabu sana, kama mlivyoziona. Hakuna hata wakati mmoja ambapo hizo ishara zimekosea.

Ni za kweli kabisa, maana ni Mungu. Maelfu kumi, mara maelfu, mara maelfu, wala hakuna hata moja la hayo linaloweza kukosea.

⁴³ Wanaliita “ibilisi.” Wanaliita kila kitu. Wengine wanasema jambo moja na lingine.

⁴⁴ Lakini Yesu alisema, “Kama wamemwita Bwana wa nyumba, ‘Beelzebuli,’ ni zaidi sana vipi watawaita wale wa wanafunzi Wake?” Kwa hiyo Yesu alisema, “Mwayachunguza Maandiko, ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele; Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.”

⁴⁵ Sasa, si kwamba hazitanishuhudia mimi; mimi ni mwanadamu. Bali Ujumbe uliotoka, unashuhudia juu ya jambo Hilo. Sasa, Mungu hatumi mambo ya ajabu sana ili kwamba tu aonyeshe ya kwamba Yeye ni Mungu. Mungu hutuma jambo la ajabu sana kufanya hivi: kutangaza jambo fulani. Huduma inatokea na mambo ya ajabu sana, na yote . . . baada ya mambo yote ya kimwili na upuuzi wote ambao unaufuata.

⁴⁶ Niliposoma juu ya Martin Luther, hivi majuzi, kilisema, “Halikuwa jambo la kushangaza kwamba yeye angeweza—yeye angeweza kuchukua na kupinga kanisa Katoliki na akubaliwe. Jambo la ajabu sana la Martin Luther, lilikuwa, yeye angeweza kusimama imara mbele ya ushupavu wote wa dini uliofuata yale matengenezo.”

⁴⁷ Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya. Kuna kila kitu kinachoendelea, na hicho kinaweka mizuka mbele yenu ndugu. Lakini, kumbukeni, ile Nuru ya kweli, wakati inapochomoza, inatowesha mbali mizuka hiyo yote. Unaona? Ilifanya, inaiabisha mizuka. Inaiweka pepepe. Na kwa hiyo tunajua kwamba mahali mambo ya ajabu sana yanapotendeka, kundi mchanganyiko daima huyafuatilia.

⁴⁸ Musa alifanya mambo ya ajabu sana. Nalo hilo hapo likaingia nyikani, Kora alijaribu kusema, “Vema, sasa, wewe unajaribu kusema wewe ndiwe pekee unayeweza kufanya jambo hili. Kuna watu wengine walio watakatifu mbali na wewe.”

⁴⁹ Mnajua kile kilichotukia, sivyo? Mungu alisema, “Hebu jitenge tu nao.” Unaona?

⁵⁰ Unaona, daima tumekuwa na mambo hayo. Wakati ishara za kimbinguni zikitendeka, waigaji hufuatilia jambo Hilo. Inapaswa kuwa hivyo. Na huko kuiga ndiko kunakoleta ninii, kama . . .

⁵¹ Kama ilivyokuwa Mbunge Upshaw. Mjane wake aliruka kwa ndege, jana usiku, apate kuhudhuria mkutano hapa. Mbunge huyo aliponywa kwenye hizo ibada. Nyote mnafahamu. Daima alikuwa na tamshi hili, “Huwezi kuwa kitu usicho.” Hiyo ni kweli kabisa. Huwezi kuwa kitu ambacho wewe—wewe sivyo ulivyo.

⁵² Kama tungeweza kuchukua kitu kama simfoni kuu, tungeweza tu kufuata mapigo yake vile huyo Mtunzi wake anavyoipiga Hiyo, tungeweza kuona. Sasa, tu—tunakuja kufikia wazo hili, ya kwamba saa tunayoishi, wakati tulimo sasa, ni kwamba tumefikia mahali ambapo tunamwangelia Mungu.

⁵³ Wakati ninyi ndugu awali mlipoanza, watengenezaji wenu, ule uamsho wa kipentekoste, miaka kadhaa iliyopita, wakati kule kurudishwa kwa karama, kule kunena kwa lugha, na mambo mengi yaliyoingia kanisani, ilikuwa Mungu akirudisha karama mbalimbali kanisani. Mnakumbuka, nyote mlikuwa na matengenezo, pia. Baba zenu walikuwa nayo. Ilikuwa ni vigumu kujiondoa kwa Presbiteri, Lutheri, Baptisti, na kadhalika, katika matengenezo hayo. Wanazarayo walikuwa kwenye upeo wa kuchanua kwao katika nyakati hizo, vivyo hivyo na Wapilgrim Holiness; waliukataa ujumbe wenu. Ni nini kilichowapata? Unaona mahali walipo leo? Sasa, kumbukeni, tunaweza kufanya jambo lile lile. Loo, naam.

⁵⁴ Wakati kanisa linapounda madhehebu, ujumbe unapoundwa madhehebu, unaingia kwenye rafu wala hauinuki tena. Sasa, ninyi ni wanahistoria hapa; ninamjua mmoja wenu, mnaona. Na hiyo ni kweli. Hauinuki tena, wakati unapoundwa madhehebu.

⁵⁵ Ukatoliki ulikuwa ndio madhehebu ya kwanza; unaitwa, katika Biblia, “kahaba,” ulikuwa, “MAMA WA MAKAHABA,” jambo lile lile, madhehebu. Je! mnaona mahali yote yanapoishia tena, hapa kwenye Baraza la Ekumeni?

⁵⁶ Sasa nimetolewa nje kwa sababu ya jambo hilo, miongoni mwa madhehebu. Hao ndugu hawatambui wanalofanya. Si mimi; mimi sijatolewa nje. Wao wanalitoa Neno nje. Biblia ilisema, katika Wakati huu wa Laodikia, ya kwamba Kristo alikuwa nje ya kanisa, akibisha, akijaribu kurudi ndani. Kamwe hapajakuwa na wakati kama huo; akiwa yuko huko nje.

⁵⁷ Maana, hakutakuwa na nyakati zingine za kanisa. Huu ndio mwisho wake. Laodikia ulikuwa ndio wakati wa mwisho, na Pentekoste ndio huo Wakati wa Laodikia, nasi tunajua jambo hilo, hakutakuwa na mengine juu ya Pentekoste. Ndiyo hivyo.

⁵⁸ Kama vile mtu. Mwingine, hakuna kiumbe kilichopata kutokea kwenye ivolusheni yake, kikija kufikia kwenye spishi bora kuliko—kuliko mwanadamu, kwa kuwa mtu yuko katika mfano wa Mungu Ambaye alimwumba. Kamwe hakutakuwa na kitu kingine kilicho juu zaidi. Hili ni . . . Neno lisingeruhusu jambo hilo liende mbali zaidi, maana Yeye ni Neno.

⁵⁹ Na wala Neno haliwezi kupanda juu ya Wakati wowote wa Kanisa la Laodikia. Nasi tunawaona, kila mmoja, pale. Yesu akiwa yuko nje ya kanisa, akijaribu kuingia ndani tena. Unaona?

⁶⁰ Hivyo ndivyo walivyomfanyia wakati alipokuwa hapa, mara ya kwanza. Yeye ni Neno. Na, Neno, Yeye alikuwa lile Neno. Wao

wanasema, “Tuna Neno!” Mafarisayo walisema, “Tuna Neno!” Lakini, Neno halisi la kweli, walikuwa wanalikataa.

⁶¹ Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Mwayachunguza Maandiko, Hayo ndiyo yanayonishuhudia.”

⁶² Leo, tunaweza kuangalia nyuma na kusema, “Walikuwaje vipofu hivyo?” Nashangaa kama, siku moja, hatutaangalia nyuma na kusema, “*Sisi* tulikuwaje vipofu hivi?” Unaona? Unaona? Haina budi kuwa hivyo, ndugu. Ni vibaya sana, bali haina budi kuwa hivyo. Sisemi “vibaya sana,” simaanishi namna hiyo. Mungu anajua analofanya. Unaona? Wao hawajui, wao. . . Neno ndilo wanalolikataa, Neno lililodhihirishwa, ahadi iliyodhihirishwa, ahadi kwa siku hii. Na sababu ya kufanyika hivyo, ni kwa kuwa watu wanaishi katika mmweko wa nuru nyingine.

⁶³ Wizi mkubwa sana uliopata kufanywa, ulikuwa ni huko Uingereza, si muda mrefu uliopita, ulifanywa kwa nuru ya uongo, wizi wa dola milioni saba. Ulimwengu haujapata kusikia juu ya wizi kama huo, Scotland Yard isingeweza kuufuatilia. Huo ulikuwa ndio wizi mkubwa sana ulimwengu uliopata kuwa nao, ulifanywa kwa nuru bandia.

⁶⁴ Hebu niseme hivi, ndugu, nikiwa na upendo moyoni mwangu kwa ajili ya mwanadamu. Mungu anajua hilo. Wizi mkubwa sana kanisa liliwahi kuibiwa ulifanywa kwa nuru ya uongo, pia, kuishi katika mng’ao wa wakati mwingine. Yale Luther, Martin Luther, Wesley, ama baadhi ya mababa wetu kamili wa Kipentekoste waliyosema. Unaona? Huo si leo. *Hii* hapa ahadi ya siku hizi, hili hapa Neno. Nanyi mnasema, “Vema, umelifasiri vibaya.” Mungu hujifasiria Mwenyewe, wakati anapolidhihirisha.

⁶⁵ Vipi kama wangelibaambia mababa wa Kipentekoste hapa nyuma, miaka hamsini iliyopita, ya kwamba walilifasiri Neno vibaya, hakuna kitu kama kunena kwa lugha? Hawakuvumilia jambo hilo. Mungu alifasiri Neno Lake Mwenyewe. Petro alisema, kwenye ile Siku ya Pentekoste, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Wangewezaje kujitoa kwenye jambo hilo? Linajifasiri lenyewe. Unaona? Halihitaji fasiri yoyote.

⁶⁶ Na, leo, wakati huu tunaishi sasa, kuna Mti wa Bibi-arusi unaojitokeza. Unaona? Hakika, huo Mti umejitokeza.

⁶⁷ Na hao, mara walipounda madhehebu, hawakuweza kupiga hatua nyingine mbele. Na ni jambo gani linalotukia? Wanaunda madhehebu na wanajitenga, ndipo hilo tawi linakatwa. Kulingana na Yohana Mtakatifu, mlango wa 15, Yeye huyakatilia mbali. Hayatumiki tena.

⁶⁸ Lakini katika moyo wa Mti huo kunatokea tunda, papo hapo juu yake. Wakati mti huo ukiwa umekomaa kabisa, hauwezi kuendelea kukua tena; papo hapo juu yake. Wakati wa mwisho wa kanisa ndio huu. Umekomaa kabisa. Ni Mti wa Bibi-arusi. Yesu alikuwa ndiye ule Mti wa Uzima tangu bustani ya Edeni. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye alikuwa ndio Mti ule wa Uzima.

⁶⁹ Kulikuwa na mti kwenye ile bustani, na mmoja wao ulikuwa ninii, kama uliugusa. . . Sasa tuna tofauti zetu juu ya jambo hilo, kwa hiyo sitaingilia hilo, lakini hebu na tuseme ulikuwa ni mti wa kutotii. Na mara walipougusa huo mti, watu wote ilibidi wafe. Ndipo iliwabidi kuwaondosha kwenye Mti huu mwingine; maana, kama wakila Mti huu wa Uzima, wote wangeishi, wakijua mema na mabaya. Hiyo ni kweli. Mnajua hilo, kama wahudumu. Tuna mawazo yetu juu ya jambo hilo, na huenda tungetofautiana kwamba mti huo ulikuwa ni kitu gani.

⁷⁰ Lakini sote tunaweza kujua ya kwamba Kristo ndiye Mti huo wa Uzima. Kwa kuwa, siku moja kwenye yubile kule, wakati walipokuwa wakinywa na kufurahi, Yesu alisema juu ya yale Maji, alisema ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye “Ule Mwamba uliokuwa jangwani.”

Wao wakasema, “Baba zetu walikula mana jangwani.”

⁷¹ Ndipo akasema, “Na wote, kila mmoja wao, amekufa. Bali Mimi Ndimi ule Mkate wa Uzima, amina, ule Mti wa Uzima ulioshuka kutoka kwa Mungu kutoka Mbinguni. Yeye alaye huu Uzi- . . . Chakula hiki, hatakufa kabisa.” Hicho ndicho Chakula cha Uzima.

⁷² Sasa, kuufanyia mzaha, Warumi walimsulubisha mtini. “Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti,” kumfanyia mzaha Mwana wa Mungu. Yeye alidharauliwa, alikataliwa. Alikuwa toka Mbingu za juu kabisa, na akawa duni kabisa duniani. Wakati alipokuwa hapa, alikwenda kwenye mji ulio chini sana. Mtu aliye mfupi kuliko wote mjini ilibidi aangalie chini apate kumwona; Zakayo. Alipewa jina lililo duni kuliko yote. Alitendewa mabaya kuliko wote, na akaangikwa juu ya . . . akafa kifo kikatili sana ambacho mtu angeweza kufa. Hivyo ndivyo watu walivyomwazia Yeye. Hivyo ndivyo dunia ilivyomwazia Yeye.

⁷³ Lakini Mungu alimwinua juu sana mpaka inambidi kuangalia chini apate kuona Mbinguni; akampa jina lililo juu ya kila jina, ambapo kila kitu kilichoko Mbinguni na duniani kinaitwa kwa Yeye. Hayo ndiyo Mungu aliyowazia juu ya jambo hilo, unaona. Kama sisi ni wana wa Mungu, sifa za mawazo Yake kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, tutamwazia vivyo hivyo. Pia kumbukeni, ndugu, Yeye ni Neno. Mnaona? Ujumbe daima hufuata mambo ya ajabu sana.

⁷⁴ Yesu, kama mwalimu kijana, wakati alipoanza kuhubiri, akiwaponya wagonjwa, kila mtu alimtaka kanisani mwao. Mnajua jambo hilo. Lakini hayo yalikuwa tu ni mambo ya ajabu sana, yale aliyokuwa nayo, anayatenda, aliyavutia macho ya watu. Lakini siku moja aliketi akaanza kuzungumza nao, ikaja huduma ya kufuata mambo ya ajabu sana, ndipo hakuna mtu aliyemtaka wakati huo. Ni jambo baya sana, bali li—linajirudia tu. Mtafahamu kutoka hapo na kuendelea.

⁷⁵ Hebu na tusome hapa katika Biblia ya kale iliyobarikiwa, kidogo tu, kwa ajili ya mazungumzo mafupi asubuhi ya leo, Bwana akipenda, hebu na tusome kutoka katika Kitabu cha YOSHUA, mlango wa 10, na kuanzia cha 12, kifungu cha 12.

⁷⁶ Na sasa tunatoka hapa saa ngapi? Tunapaswa kutoka hapa saa ngapi? [Mtu fulani anasema, “Hakuna wakati uliopangwa.”—Mh.] Tuseme, vema, nitasema ni mnamo dakika kumi na tano, ishirini. Hizo zitasosha? Zitakuwa sawa? Vema, hebu kidogo. [“Hakuna wakati uliopangwa.”]

Ndipo YOSHUA akanena na BWANA katika siku hiyo ambayo BWANA aliwatoa Waamori mbele ya wana wa Israeli; akasema mbele ya macho ya Israeli, Wewe Jua, simama kimya, simama juu ya Gibeoni; na wewe Mwezi, simama katika bonde la Aiyaloni.

Ndipo jua likasimama, na mwezi ukatulia, hata hilo taifa lilipokuwa limekwisha jipatiliza juu ya adui zao. Hayo, je! hayakuandikwa ndani ya kitabu cha Yashari? Basi jua likasimama kimya katikati ya mbingu, wala halikufanya haraka kuchwa kama muda wa siku nzima.

⁷⁷ Sasa nitachukua tu fungu dogo kutoka hapo, kwa maana niliwaambia nitaninii...siwezi kuzungumza, bali nafikiri mnaelewa ninalomaanisha, kwa sasa. Nami nipo hapa kuwaunga mkono, kuwasaidia, kumkumbatia Yesu Kristo. Si kukumbatia madhehebu, si kukumbatia watu wa duniani; bali kumkumbatia Yesu Kristo, Ambaye ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, Mungu aliyedhihirishwa. Si yale tu mtu fulani anayofasiri; Mungu akijifasiria Mwenyewe, Mungu akithibitisha kwamba ni kitu gani. Yeye huthibitisha kile Yeye alichu. Laiti Mafarisayo wangelikuwa wameona jambo hilo, laiti wangelikuwa tu wameyasoma Maandiko ambapo yalisema mambo haya, wangeliona ya kwamba Mungu alikuwa akidhihirisha Neno Lake kwa Yesu Kristo. Yeye alikuwa ndiye hilo Neno, na Yeye angali ni Neno.

⁷⁸ Sasa somo hili ninataka kulichukua kwa dakika kumi na tano hivi, nami nitajaribu kufanya mazungumzo yangu... Mimi hurekodi kanda, kama vile ninyi nyote mnavyosikia, saa tatu na saa nne. Lakini kanda hiyo ni juu ya somo fulani, unaona. Na katika makanisa yenu, mimi hujaribu kufanya mazungumzo yangu, usiku, kama dakika thelathini, ili kwamba niweze

kushughulikia mstari wa maombi, wala sitawachosha watu sana, kisha nirudi. Nina hakika mnapenda hilo bora zaidi. Nilikuwa nikikaa kwa saa kadhaa na kuingia kama saa tano na nusu na saa sita, na sasa ninajaribu na hufanya ibada yangu kama dakika arobaini na tano hadi saa moja.

⁷⁹ Nataka kuchukua somo hapa la: *Kitendawili*, neno hilo tu, kitendawili.

⁸⁰ Na sikujua nitakula kiamshakinywa. Kwa kawaida sisi hula kiamshakinywa, lakini nilidhani labda kingekuja labda Jumamosi, ama kitu kama hicho. Naye Ndugu Borders aliniambia, jana usiku, saa zilizoenda, ya kwamba kingekuwa ni leo asubuhi, kwa hiyo niliandika tu Maandiko machache hapa ambayo nilidhani ningeyarejea kwa dakika chache.

⁸¹ Sasa, *kitendawili*, Webster inasema ni “kitu ambacho hakiaminiki, bali ni kweli.” Yaani ni kitu ambacho hakuna mtu anayeweza kuelezea. Kiko nje ya milki ya maarifa ya binadamu, bali hata hivyo ni kweli. Kitendawili! Na sasa tunaona, ya kwamba kama ungesoma katika—katika Waebrania, mlango wa 11 na kifungu cha 3, ya kwamba ulimwengu huu wenyewe ni kitendawili.

⁸² Majuma machache yaliyopita, katika mikutano yetu katika Jiji la New York, nilitoka usiku mmoja kutoka katika Jumba la Mikutano la Morris, nasi tulikuwa tukishuka kwenda barabarani, mimi pamoja na mwanangu. Nasi—nasi tukawaangalia watu, na kulikuwa na maelfu tu, na wanaume wenye nywele kama za wanawake, mwajua, wanazoita mlevi sugu, na—na herini, na nguo zilizobana sana; na—na watoto wa kizungu na machotara, mnajua ninachomaanisha, wanaume na wanawake pamoja. Na—nao, nao. . .

⁸³ Mwanamke mmoja maskini alianguka barabarani, hakuna mtu aliyemwokota, waliendelea tu. Nami nikamsaidia kuokota machungwa yake, basi nikaokota namna hiyo, maskini kizee chenye umri wa miaka kama sabini. Na—naye akaniangalia kwa mshangao sana, akashuka akaenda zake barabarani.

⁸⁴ Nikazungumza na dereva wa tekisi juu ya jambo hilo. Akasema, “Bwana, mtu yeyote anapokuja New York, na anatenda kana kwamba ana akili timamu,” akasema, “tunajua yeye ni mgeni.” Unaona? Kasema, “Hao ni watu wazuri,” kasema, “bali wanaingia tu kwenye mkondo huo.” Kasema, “Ukimchukua mtu anayekuja hapa, haitachukua muda kabla hujaingia katika hali ile ile. Anakuja hapa, anajaribu kufanya kila kitu.” Kasema, “Ungeweza kulala pale na ufe kwenye barabara hiyo, kwa mshtuko wa moyo, mtu fulani atafikiri wewe ulikuwa mlevi. Wasingekugusa hata; watakuacha ulale pale na ufe.” Unaona, hawamaanishi kuwa namna hiyo. Ni kuingia tu kwenye mkondo huo.

⁸⁵ Na hivyo ndivyo tunavyofanya, ndugu, katika maisha yetu ya kanisa. Tunaingia katika mkondo wa kanuni fulani moja ya imani, ama kitu fulani kimoja, nasi tunakaa hapo. Unaona, tunabembea pamoja na wengine wote. Tunabembea pamoja na madhehebu yetu.

⁸⁶ Tunabembea pamoja na jumuiya yetu. Ni jambo la kawaida tu. Hebu paka vipandio vyako rangi nyekundu, kisha uangalie vile jirani yako atakavyofanya. Watafanya hivyo, pia. A-ha. Hebu mmoja wenu ninyi akina dada apate nguo ya aina fulani, ama kofia, na uangalie jinsi majirani zako watakavyofanya. Unaona? Ni u—ni uigaji. Ni wakati wa kujilinganisha.

⁸⁷ Hatujali kama suruali zetu zinalingana na makoti yetu. Tunataka ujuzi wetu ulingane na Neno, unaona, na Mungu.

⁸⁸ Lakini tulipokuwa tukitembea huko mtaani, Billy aliniambia, akasema, “Baba, Mungu anajuaje hao wote ni akina nani?”

⁸⁹ Nikasema, “Vema, mwanangu, angalia moja kwa moja kuelekea mbinguni.” Kisha nikasema, “Unaona zile nyota mbili ndogo huko juu, karibu kugusana?”

“Naam.”

⁹⁰ Nikasema, “Kama moja ya hizo, sayansi inatwambia, kama moja ya hizo ingeanza kusafiri kuelekea duniani, maili milioni moja kwa saa, ingechukua miaka milioni nyingi kufika hapa. Hivyo ndivyo kadiri ilivyo mbali. Na hata hivyo hizo nyota mbili zinakaribiana moja kwa nyingine kuliko sisi tunavyokaribiana na nyota hiyo, ama labda tuko karibu na hiyo nyota kuliko zilivyo karibu, kwetu.”

Akasema, “Mungu anafanyaje jambo hilo?”

Nikasema, “Yeye hana kikomo.” Unaona?

⁹¹ Ndiyo kwanza tusikie mhadhara kutoka kwa Einstein, juu ya hili kundi la nyota na kilimia. Naye alisema, “Kama m—mtu angeweza kusafiri toka duniani. . .” moja ya hotuba zake kuu, zile za mwisho. “Kama mtu angeweza kusafiri toka duniani kwa mwendo wa nuru, hiyo ni mia nane na . . . maili mia moja na themanini na sita elfu kwa sekunde; maili mia moja na themanini na sita elfu kwa sekunde, na angesafiri miaka milioni mia moja na hamsini ya nuru, angefika kule. Ndipo ingemchukua maili milioni elfu moja na hamsini ya nuru kurudi.” Hiyo ingekuwa mabilioni kadhaa ya miaka, ungeweza kuandika safu ya tisa-tisa kuizunguka dunia na usiweze kuihesabu, katika kuzungumza kuhusu miaka. Unajua atakuwa ameondoka duniani kwa muda gani? Miaka hamsini, katika wakati wetu.

⁹² Tuna harakaharaka sana! Vipi kama maskini siafu angalianza safari ya kutoka Tucson, asafiri kuja hapa Bakersfield, unafikiri angefika wapi katika miaka arobaini? Labda ni nusu maili. Unaona, inamaanisha jambo kubwa sana

kwake; kwetu, inamaanisha saa kumi na mbili za kuendesha gari; kwa ndege aina ya jeti, ni sekunde chache tu, kwa Mungu, si kitu.

⁹³ Yesu alikufa jana alasiri, alisulibiwa. Paulo alikufa jana, “Miaka elfu moja ni kama siku moja kwa Mungu,” kama ilivyo, hata si hayo tu, bali ukitaka kuhesabu wakati. Kwa hiyo hao mitume, na kadhalika, walikufa jana. Sisi tunaharakisha; hatuna ila muda mfupi tu wa kukaa hapa. Ndipo unawazia, unapoangalia Umilele. . .

⁹⁴ Einstein, yule mwanafalsafa mkuu alisema, ama yule mwanasayansi mkuu alisema, ya kwamba, “Kuna njia moja tu yenye busara ya kuelezea asili ya dunia hii, iliyopatikana katika Waebrania, mlango wa 11 na kifungu cha 3, ‘Kwa imani tunafahamu Mungu aliumba ulimwengu, kutokana na vitu visivyo- . . .’ Aliunena ukawa.”

⁹⁵ Unasimamaje mbinguni, wala hautoki kamwe kwenye obiti yake? Jinsi ambavyo kila kitu mbinguni, na hicho kilimia, kama moja ya hizo nyota ingesogea. . . Ninajua unatoka nje usiku na kusema, “Nimeona nyota ikihama.” La, uliona nuru ya hali hewa. Nyota haisogei. Kama nyota hiyo ingesogea, tungsogea pamoja nayo. Kila kitu mbinguni kiko katika upatanifu sana, vinashikana pamoja.

⁹⁶ Vipi kama wanadamu wanalikuwa namna hiyo, kulishikilia kanisa pamoja? Kwamba sote tungekuwa katika upatanifu pamoja na Neno. Unaona? Kuna njia moja tu, kumwacha Mungu awe mfasiri Wake Mwenyewe, na tutakuwa katika upatanifu. Unaona? Mungu ndiye anayejifasiria Hilo.

⁹⁷ Sasa tunaona ya kwamba katika jambo hili ni kitendawili tu. Hapana shaka ila kwamba ni moja ya vitendawili vikubwa. Sasa, kumekuwa na vitendawili vingi sana, tunaposonga mbele. Mambo mengi, ni—ni kitu kisichoaminika, bali ni kweli.

⁹⁸ Katika siku za Nuhu, kumbukeni, haikuwa imewahi kunyesha juu ya nchi. Hakujawa na kitu kama mvua. Dunia ilisimama wima, sawa tu na jua. Kutokuamini na kuasi ndiko kulikoivuruga, kunaifanya iinaume nyuma, na kusababisha hewa yenye joto na yenye baridi kuinua mvuke kutoka baharini, na kufanya mvua inyeshe. Haijawahi kunyesha juu ya nchi. Na huyu hapa anatokea mtu, akisema kwamba itanyesha. Jambo la kushangaza, bali lilikuwa ni Neno la Bwana. Loo, ninaweza kusikia sayansi. . .

⁹⁹ Mnasema, “Vema, sasa, unajuaje walikuwa na sayansi?” Walijenga mapiramidi katika siku hizo. Tusingeweza kuyajenga leo. La. Hatuna vifaa hivyo. Hatuna vitu vya kuyajenga navyo, wala hatuna mitambo ya kuinua majabali hayo huko juu. Lingali ni jambo la kushangaza, kwa ulimwengu. Wao waliyajenga.

¹⁰⁰ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.

Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁰¹ Na, ndugu, jambo dogo kwa kuunga mkono ninaloweza kuingiza hapa kwa dakika moja. Petro alinukuu, katika Petro wa Kwanza, yeye alisema, “Ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji.” Watu wanane! Halmashauri ya Ekumeni ya makumi milioni ni ya nini? Unaona, hiyo haiokoi. Ni Neno. Mungu ndilo analookoa nalo. “Watu wanane waliokolewa kwa maji, katika siku za Nuhu.”

Angalia wale waliokolewa katika siku za Lutu.

¹⁰² Angalia wale waliomalizia safari katika ile safari ya jangwani; wawili, Yoshua na Kaleb. Unaona?

¹⁰³ “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁰⁴ Wakati mkuu wa kisayansi! Unaona? Na, hapana shaka, wangetuma vyombo angani na kusema, kwa rada, na kusema, “Hakuna maji huko juu. Yanatoka wapi?”

¹⁰⁵ Mungu alisema, “Yatakuwepo.” Hilo lilitosha kabisa. Naye Nuhu aliamini hilo, na akaiokea nyumba yake.

¹⁰⁶ Kumbukeni, Mungu huwajaribu watu Wake ambao wanaamini Neno Lake. Mahali Mungu alipo, daima kuna kitendawili, maana Yeye hufanya vitu ambavyo haviaminiki kwa mawazo ya kibinadamu. Je! ulifahamu hilo? Sote tunajua hilo. Haviaminiki kwa mawazo ya kibinadamu! Naye huwajaribu hao wanadamu wanaobashiri kitendawili hiki. Yeye huwapa majaribu.

¹⁰⁷ Kamwe Yeye haachi wala kubadili njia Yake. Mungu kamwe habadilishi mfumo Wake. Je! mnajua jambo hilo, ndugu? Hakika, mnajua. Yeye kamwe habadilishi mfumo Wake. Daima Yeye huuendeleza katika mwendeleo, jinsi alivyoanza.

¹⁰⁸ Yeye kamwe hakushughulika na ulimwengu, ila tu chini ya mahubiri, akiwa na mtu mmoja, Nuhu. Kamwe hajawahi kuwa na wanne walioshuka kwenda kuwakomboa, wala madhehebu, katika siku za Musa. Kamwe Yeye hajawi kuwa na wawili duniani katika wakati uo huo. Kila mmoja wetu ni tofauti mmoja kwa mwingine, sura zetu, tabia zetu. Mungu anamshikilia tu... Kitu tu anachohitaji ni mtu mmoja ambaye anaweza kumwongoza; ambaye ni mfano Wake. Alifanya jambo hilo kwa Musa. Alifanya hivyo daima.

¹⁰⁹ Wakati Eliya na Elisha walipokuwa duniani, wote wawili wasingeweza kuwapo kwa wakati mmoja. Mmoja alitwaliwa, huyo mwingine alitwaa joho la huyo mwenzake.

¹¹⁰ Wakati Yohana alipokuja duniani, Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa kwa saa hiyo. Tunajua hilo. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Kwa sababu gani? Isaya alisema, “Kutakuwa na sauti ya mtu aliaye nyikani.”

Malaki, yule nabii wa mwisho, alisema, “Angalia, ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia mbele za watu.” Sasa, hiyo haikuwa ni Malaki 4; hiyo ilikuwa ni Malaki 3. Yohana alikuwa ndiye Eliya wa Malaki 3, si Malaki 4.

¹¹¹ Kwa sababu, wakati Malaki 4, wakati unabii huo utakapotokea, ulimwengu utachomwa kwa moto mkali, na wenye haki watatembea katika ule Utawala wa Miaka Elfu, juu ya majivu. Wala jambo hilo halikutukia katika siku za Yohana.

¹¹² Katika Mathayo 11, tunaona ya kwamba wakati Yohana alipowatuma wanafunzi wake huko chini ambako... Yohana alimpa Yesu he—heshima ya chini sana aliyoweza kumpa, baada ya yeye kuona ishara hiyo juu Yake. Naye akasema, “Huyo Ndiye. Yeye aliyeniambia huko jangwani niende nikabatize katika maji, alisema, ‘Yule utakayeona Roho akishuka na kukaa, Yeye atabatiza kwa Roho Mtakatifu.’” Yeye alisema alikuwa na hakika ya jambo hilo. Aliona ile ishara. Ndipo baada ya jicho lake la tai kuingia utando, huko gerezeni, yeye alisema, “Nendeni mkamwulize kama kweli Yeye Ndiye, ama ni mwingine.” Hiyo ilikuwa ni kutolichukulia Neno uzito.

¹¹³ Lakini Yesu alijua jambo hilo. Alimpa Yohana heshima kubwa. Alisema, “Mlitoka kwenda kumwona nani, mtu aliyevaa mavazi mororo? Hao hawashiki upanga. Wao wanawabusu watoto wachanga na kuzika wafu, wako kwenye majumba ya wafalme.” Kasema, “Mlitoka kwenda kuona nini, unyasi unaotikiswa na upepo wowote? Wakati shirika moja linapompa zaidi kidogo ya hilo lingine, ama jumuiya fulani, yeye ataenda kwenye jumuiya hiyo maana...? Si Yohana.

¹¹⁴ Kasema, “Mlitoka kwenda kuona nini, nabii?” Kasema, “Nawaambia, na zaidi ya nabii.” Yeye alikuwa zaidi ya nabii. Alikuwa ni mjumbe wa agano. Alikuwa ndiye lile pengo. Alikuwa ndiye jiwe muhimu kati ya torati na neema. “Mlitoka kwenda kuona nani, nabii? Nami nawaambia, zaidi ya nabii.”

¹¹⁵ Akasema, “Yeye alikuwa taa iwakayo na kung’aa, kwa muda.” Kwa nini? Alikuwa ni lile Neno lililofanywa taa. Alikuwa Neno lililodhihirishwa.

¹¹⁶ Ndipo wakati alipojitokeza jukwaani, yeye alisema, “Sina budi kupungua: Yeye hana budi kuzidi.” Wawili wa hao wasingekaa katika wakati uo huo. Ilimbidi Yohana kuondoka; Yesu akabaki. Unaona? Ndivyo ilivyo daima.

¹¹⁷ Mungu alifanya jambo hilo katika siku za Nuhu, nasi tunaona basi ya kwamba hiyo ilikuwa ni ajabu kuu sana. Lilikuwa ni jambo fulani, vema, ilikuwa ni kitendawili, ya kwamba Mungu aliifanya ile safina kuelea; wakati ulimwengu wote ulipokuwa ukiyumbayumba, kukiwa na mawimbi yaliyokuwa labda ni makubwa kuliko milima ilivyo leo. Wakati ilipobembea kutoka kwa ninii yake... Wakati nyota ziliporudi

nyuma, ama chochote kilichotukia, na dunia hiyo ikatoka kwenye obiti yake, ikabembea ikatoka hapo, na hayo mawimbi makubwa; bila shaka kilikuwa ni kitendawili ya kwamba maskini ile meli ya kale ya mbao ingeweza kuyumbayumba, kwa muda wa siku arobaini mchana na usiku, juu ya hiyo, katika maji hayo. Ilikuwa ni kitendawili. Il kuwa ni kitendawili, ya kwamba Mungu angeweza kuleta maji kutoka mbinguni, wakati hakukuwa na maji kule ya kuletwa.

¹¹⁸ Lakini Yeye anaweza kutengeneza hali ya mambo iendane na Neno Lake. Yeye angali, kama vile katika Mwanzo 22 *Yehova-Yire*, “Bwana anaweza kujipatia dhabihu.” Unaona? Yeye hudumu. Hilo ni moja ya majina Yake ambatani, ya ukombozi.

¹¹⁹ Ilikuwa ni kitendawili, wakati wana wa Kiebrania walipotupwa kwenye tanuru la moto mkali. Jinsi ambavyo watu hao watatu wangeweza kutembea waingie kwenye tanuru, lenye joto sana hivi kwamba lile joto kali liliwaua wale watu waliokuwa wakiwasukuma waingie humo. Na hata hivyo walikaa humo, ulichofanya ni kuwafungua tu. Hilo ndilo jambo pekee ulilofanya. Unaona? Uliwafungua kutokana na vifungo ambavyo walikuwa wamefungwa navyo. Ilikuwa ni kitendawili.

¹²⁰ Mara nyingine, katika maisha yetu wenyewe, kitendawili hicho hujirudia. Mara nyingine mtu unaletwa kwenye shindano la kuamua, ambapo inakubidi kufanya uamuzi. Inakubidi kusimama na uamuzi huo, kama wao walivyofanya, na yote yanatenda kazi kwa pamoja kwa manufaa mema. Ulifanya nini? Haukuwadhuru kamwe. Uliwafungua. Mara nyingine tunajikuta kwenye hali hiyo. Jambo la kwanza tulilo nalo, kama tu vile mtu anayekufa maji mtoni, inakubidi kumtoa mtu huyo mtoni kabla ya kuweza kuutoa mto kutoka katika mtu huyo. Naam. Na hilo ndilo jambo ambalo mtu anapaswa kufanya wakati mwingine, ni kujitokeza na kuchukua msimamo wake, atoe kitu hicho nje. Na kumtoa kwenye kitu hi—hicho, kusudi aweze kutoa kitu hicho ndani yake.

¹²¹ Hivyo ndivyo ilivyowabidi wana wa Kiebrania kufanya. Ilibidi watoke kwenye ule moto, na ndipo Mungu akafanya kitendawili kutendeka.

¹²² Daudi, tunamwona Daudi, mtoto mdogo tu, mvulana tu mwenye kombeo; si mkuki, upanga. Alikuwa amewekwa kuwachunga kondoo, kuwachunga. Neno la baba yake lilikuwa, “kuwachunga kondoo.” Alikuwa mchungaji.

¹²³ Ndugu, hivyo ndivyo tunavyosimama asubuhi ya leo. Sisi ni wachungaji. Hatuhitaji elimu ya chuoni. Hatuhitaji kitita cha theolojia. Tunahitaji Neno la Baba. Huenda likaonekana ni jambo rahisi. Na wakati dubu ama mwizi anapokuja na kumchukua mmoja wa kondoo za Baba, na kuzibeba katika namna fulani ya itikadi, ni kitu kidogo sana tunachoonekana

tukiwa nacho. Kinachekwa, bali ni ninii, loo, lina nguvu sana wakati Mungu akiwa nyuma yake. Nenda ukamtafute; umrudishe!

¹²⁴ Jinsi ambavyo Daudi aliweza kuchukua lile kombeo na kumwua simba! Nimewinda simba. Jamani! Nimekaa kwenye kilima hapa, siku moja, na, nadhani, umbali wa nusu maili... Mmewasikia wakinguruma hapa, kwenye sarakasi hizi. Bali unapaswa kumsikia wa mwituni akinguruma siku moja, miamba inavingirika kutoka kilimani ambako jamaa huyo alingurumia.

¹²⁵ Na kumwona huyo mnyama mkali namna hiyo, na maskini mvulana huyu mdogo, maskini aliyeinama mgongo, jamaa mwekundu, anaenda na kumwua simba huyo, akiwa na kombeo. Hicho ni kitendawili.

¹²⁶ Ilikuwa ni kitendawili wakati mtu, mwenye vidole vya inchi kumi na nne, jina lake Goliati, shujaa tangu utoto wake, amefunikwa na silaha; jinsi ambavyo Mungu alichukua kombeo lili hili dogo na kuliangusha chini jitu hi—hilo, kwa sababu alikuwa anayapinga majeshi ya Mungu. Ilikuwa ni kitendawili.

¹²⁷ Na tunapochukua msimamo wetu, leo, wakati mtu anaposema mambo haya hayawezi kutukia, usiwe ukizozana nao. Hilo ni kosa. Usizozane nao, bali chukua Upanga. Chukua ninii... Wewe angalia kile kinachopaswa kuwa siku hii, wakati Mungu alipotoa ahadi Yake kwa ajili ya leo. Chukua *Hili* na uende, Magoliathi wote wataanguka chini Yake. Ni kitendawili. Kile Mungu anachofanya leo ni kitendawili. Yeye anawezaje, Yeye, ni Mungu tu anayeweza kufanya jambo hilo. Vema. Lile kombeo!

¹²⁸ Musa ndiye aliyekuwa amefunzwa katika he—hekima yote ya Wamisri. Aliweza kuwafundisha Wamisri sayansi, na kadhalika. Na kwa kweli ilikuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo Mungu alimtayarisha mtu huyo. Sasa angalia, elimu yake yote, kila kitu alichokuwa nacho, ilichukua miaka arobaini kumwelimisha, kisha ikamchukua Mungu miaka arobaini kuitoa ndani yake. Unaona? Unaona? Mtoe mtu majini kabla hujaweza kuyatoa maji kutoka katika mtu huyo. Unaona? Ilimchukua miaka arobaini kumtoa yale aliyokuwa amejifunza. Alikuta kwamba yale aliyokuwa nayo yasingewakomboia Israeli, na hilo ndilo kusudi la kuzaliwa kwake. Hakuwa na chaguo la jambo hilo; Mungu alimwitia jambo hilo. Na tunaona ya kwamba ilichukua miaka arobaini kuitoa kwake.

¹²⁹ Na wakati mwingine wakati mtu anapozifuata amri za Mungu kweli, yeye hufanya mambo yanayoonekana kwa namna fulani kuwa kana kwamba, nadhani, ni “wazimu,” kwa watu wengine.

¹³⁰ Yesu alihesabiwa kuwa ni “mwenda wazimu,” bali alikuwa akifanya hasa yale Baba aliyomwambia kufanya. Yeye alikuwa ni lile Neno, lililodhihirishwa. Alitwa “mwenda wazimu.”

¹³¹ Mwangalie Musa akiwa na huyu, mke wake Zipora akiketi juu ya nyumbu, na Gershomu pajani mwake; akiwa na umri wa miaka themanini, ndevu zenye mvi zikining'inia kufikia kiunoni mwake, kichwa chake chenye upara kikiwaka kwenye mbingu, akiwa na fimbo iliyopindika mkononi mwake, akishuka kwenda Misri, kuiteka. Ungeweza kuamini jambo hilo? Wao wanasema, “Unaenda wapi, Musa?”

“Ninashuka kwenda Misri, kuiteka.”

“Unajuaje utaiteka?”

“Bwana aliniambia nikaiteke.”

¹³² Kuliteka jeshi! Si jeshi tu, bali taifa. Ukweli wa mambo ni kwamba, alifanya hivyo. Hicho kilikuwa ni kitendawili. Jinsi ambavyo, akiwa na fimbo iliyopinda, alileta hukumu za Mungu juu ya Misri; na akawakomboa Israeli, akiwa na fimbo iliyopinda, si jeshi wala upanga. Kilikuwa ni kitendawili.

¹³³ Kama mtu yeyote angeangalia mambo ambayo—ambayo hayaaminiki, bali hata hivyo ni kweli, ni kitendawili wakati wao—wakati wao... wakati wanapoweza kufanya jambo hilo, wakati unapofanya jambo hilo.

¹³⁴ Sasa tunaona pia, Yoshua, hapa, ambaye tulikuwa tukinena habari zake, hapa katika—katika Yoshua 10:12, Yoshua.

¹³⁵ “Jua,” tunasema, wao wanatwambia siku hizi, “husimama kimya. Dunia huzunguka.” Wanasema, “Dunia kama ikisimama, ingedondoka. Nguvu za uvutano huishikilia kwenye nafasi yake.”

¹³⁶ Sasa, ndugu, ni kitu gani kilitukia? Yeye alilitamkia “jua kusimama kimya.”

¹³⁷ Mwalimu wangu shuleni, na—na akifundisha Biblia, alisema, “Yeye, Mungu, alifumbia macho ujinga wake.” Lakini, hata hivyo, lilisimama. Hilo ndilo lililokuwa jambo muhimu. Lilisimama.

¹³⁸ Naye anasema hapa, ya kwamba, “Lilisimama kimya kwa karibu siku nzima; na mwezi ukaning'inia juu ya Aiyaloni.” Hilo, “Jua lilisimama kimya.” Chochote alichosimamisha, mimi sijui ni nini alichosimamisha. Lakini kwa sababu ya mwanadamu kusema, “simama kimya,” na i—imeandikwa hapa, ya kwamba, “Jua lilisimama kimya.”

¹³⁹ Sayansi inathibitisha jambo hilo, ya kwamba alama fulani huko angani ingali inasema ya kwamba huo ni ukweli, inaweza kuthibitishwa kwa alama fulani angani, leo, ya kwamba jambo hilo lilitukia. Unaona? Hiyo imekuwa tu kama—kama miaka elfu mbili mia tano iliyopita, ama kitu kama hicho, miaka elfu mbili mia nane iliyopita, labda, ambapo hilo lilifanyika. Haijaninii, alama hiyo haijapata kuwa na wakati wa kuzifuata nyota na kadhalika, bado. Hiyo ilikuwa ninii tu... Hizo ni siku mbili tu zilizopita, kwa wakati wa Mungu, unaona, bali ile alama bado

inaonyesha. “Nalo lilisimama kimya!” Hicho ni kitendawili. Hakuna mtu angaliweza kuliwazia hilo. Kama jua . . .

¹⁴⁰ Kama dunia inazunguka, basi unasema, “Yeye aliisimamisha dunia.” Vema, kama aliisimamisha dunia, basi sayansi inasema, ya kwamba, “Nguvu za uvutano, ikizunguka, zinaishikilia kule juu, basi dunia ingalianguka, yenyewe.” Lakini iliendelea moja kwa moja kuzunguka, kwa mkono wa Mungu. Kitendawili. Kwa nini?

Loo, unasema, “Huo ulikuwa ni muda mrefu uliopita.”

¹⁴¹ Hilo ni leo, Mungu yule yule. Yesu alisema, katika Mathayo, si Mathayo, ni Marko Mtakatifu 11:22, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Huko ni kuasi maumbile, bali unapaswa kuwa na nia na kusudi kwa jambo hilo, lililo na uhusiano nalo. Angalia katika Neno kama linapaswa kufanywa, na halafu kama Mungu anakuita kufanya jambo hilo, na litatukia. Unapojua ya kwamba limenenwa katika Neno kulifanya, na halafu Mungu amekuita kulifanya, basi litatukia; kama nia na kusudi lako ni sawa, kwa Mungu. Hiyo ndiyo sababu maono hutukia, ndiyo sababu mambo yanaenda jinsi . . . Unapaswa kujua, na ujue ya kwamba Mungu aliahidi jambo hilo wakati huu.

¹⁴² “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Yeye aliahidi katika siku za mwisho, ndipo anaita kufanya hivyo. Hakuna shida. Mungu alisema hivyo. Hilo latosha. Hakika, hicho ni, hicho ni—hicho ni kitendawili. Huwezi kulielezea. Hakuna mtu anayeweza kuelezea jinsi ambavyo mambo fulani yatakavyobashiriwa na wala kamwe hakuna wakati hata mmoja yatashindwa kutukia. Ni kitendawili. Lakini Mungu alisema lifanye. Ndiyo siku yenyewe. Hiyo ndiyo siku tunayoishi.

“Jua lilisimama kimya.”

¹⁴³ Samsoni, ilikuwa ni kitendawili jinsi ambavyo aliweza kumwua simba, kwa mikono mitupu; maskini kibushuti chenye nywele za kipilipili. Alite- . . . Alikuwa ametengwa, na Mungu, alikuwa Mnadhiri, ametengwa kwa Neno la Mungu. Alikuwa ni Mnadhiri, na kwa hiyo akajitenga kwa ajili ya Neno. Wala hakuwa na mabega yenye saizi ya ule mlango pale. Mtu yeyote mwenye mabega kama hayo angeweza kumwua simba. Hilo lisingekuwa ni jambo la ajabu hata kidogo, kama alikuwa na ukubwa huo kama vile sayansi ama—ama theolojia za siku hizi, na—na wasanii wanavyojaribu kuichora picha yake. Yeye alikuwa kijitu kidogo tu, unaona, naye asingeweza kabisa kufanya jambo hilo. Bali wakati Roho wa Bwana aliposhuka juu yake, basi angeweza kulifanya.

¹⁴⁴ Huenda tukasimama peke yetu, huenda tukasimama kama mmoja ama wawili, chochote kile; wakati Roho wa Bwana

anapojaribu kuthibitisha Neno aliloahidi na kukwambia ulifanye, litatukia. Itakuwa ni kitendawili, tena. Bila shaka.

¹⁴⁵ Ilikuwa ni kitendawili wakati mtu huyu aliweza kuchukua mfupa wa taya la nyumbu, ambao aliukota kondeni. Sasa, kumbuka, vyepeo hivyo vya Wafilisti vilikuwa na unene wa kama nchi moja ya shaba. Wazia jambo hilo. Naye alikuwa na mfupa wa taya la nyumbu, ulikuwa uko huko chini nyikani.

¹⁴⁶ Uliwahi kuokota mmoja? Unaweza kuupiga teke, nao utapasukapasuka katika vipande milioni moja. Ukiugonga kwenye mwamba, karibu unakuwa unga.

¹⁴⁷ Basi akachukua mfupa huu wa taya la nyumbu huyu, na kuwapiga Wafilisti elfu moja, akavunja vyepeo vyao. Mfupa huo wa taya ulistahimilije? Kwa nini mkono wake haukuchoka? Angeweza kufanya jambo hilo, na hao ni watu waliofunzwa kutumia mikuki? Ni kitendawili. Mungu alitoa ahadi. Na mahali alipo Mungu, vitendawili daima hutukia mahali alipo Mungu. Naam, bwana.

¹⁴⁸ Hivi halikuwa ni jambo la ajabu katika siku zile wakati Mfalme Ahabu alipokuwa mfalme, na—na wa Yuda, na wa Israeli, hasa; na—na Yehoshafati, yule mtu mwenye haki, mfalme wa Yuda, wa Yuda; nao wakafanya muungano pale. Jinsi mwaminio anavyoweza kushikana na—na anayejifanya mwaminio!

¹⁴⁹ Mara nyingine mtu huingia katika shida kama hiyo, leo, wanajichanganya na watu wasioliamini Neno, na hata hivyo wanashikamana nao, wanajifunga sana, mpaka hawawezi kutoka. Wanaogopa kukubali jambo Hilo.

¹⁵⁰ Ninavutiwa na ninii wenu, ujasiri wenu ndugu. Sasa, haiwabidi kulifasiri hilo. Mnaona? Mnaona? Wanapokanusha, ama hawatajihu chochote, “liondosheni,” na hata hivyo mtachukua hatua moja kwa moja na kuudhamini. Mnaona? Ninampenda mtu wa namna hiyo. Hamuwaogopi akina Kaisari na hizo amri, mnaona. Naam.

¹⁵¹ Waaminio wakiungana na wasioamini! Na Yehoshafati alifanya hivyo wakati aliposhuka kwenda kwa Ahabu, yule mwaminio vuguvugu, mkwamia mpakani, aliwazia zaidi juu ya mambo ya burudani za ulimwengu, na mtindo mzuri wa nywele za mke wake, na kadhalika, kuliko alivyofikiria juu ya Mungu. Akamsikiliza! Nasi tunaona ya kwamba Israeli ilikuwa ni mfano halisi wa taifa hili, wakati huo; jinsi walivyoenda kule na kuwaondosha wenyeji, na kuikalia, na walikuwa na watu mashuhuri kama Daudi na Sulemani, lakini hatimaye kukainuka mtu kama Ahabu.

¹⁵² Lakini katika siku za Ahabu ndipo nabii alipojitokeza jukwaani. Mungu daima hudhihirisha Neno Lake.

¹⁵³ Nasi tunaona, basi, ya kwamba taifa hili limefanya jambo lile lile. Tuliingia, tukawafukuza Wahindi, na tukaikalilia, na tulikuwa na akina Washington na Lincoln. Lakini tunaielekea wapi sasa? Lakini Mungu angali anaweza kuwainua manabii. Yeye anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto, wakati Neno Lake linapohitaji jambo hilo. Malaki alisema tutakuwa na manabii, na tutakuwa na manabii. Watakuwa hapa. Msijali. Neno Lake litatimizwa.

Angalia, Mikaya alikuwa huko katika nchi ile.

¹⁵⁴ Na Ahabu, ili kwa namna fulani aipambe nchi, alikuwa nao kule manabii mia nne wa Kiebrania, wakiwa ni madhehebu makubwa. Wote walikuwa wamevalia vizuri, nadhifu, wenye elimu, watu wasomi, manabii wa Kiebrania, sasa, si makafiri. Manabii wa Kiebrania! Yehoshafati alifanya mapatano haya.

¹⁵⁵ Nafikiri mambo yote yanatenda kazi pamoja. Simfoni inapiga vizuri mdundo huo. Mnaona?

¹⁵⁶ Kwa hiyo akafanya mapatano, kupanda huko juu, kumteka mfalme wa Edomu na kwenda kuingia nchini, kuwateka Waashuri, kwa sababu lilionekana ni jambo zuri sana.

¹⁵⁷ Naye Yehoshafati akalipenda wazo hilo, akiwa ni mcha Mungu, akasema, “Inatupasa kumtaka shauri Bwana, sivyo?”

¹⁵⁸ Akasema, “Hilo ni sawa. Samahani, ilinipasa kuwazia jambo hilo. Naam, nina seminari hapa chini, nina walio bora sana nchini, wasomi wa hali ya juu. Wanaweza kusema ‘amina’ vizuri sana ulivyopata kusikia.” Unaona?

¹⁵⁹ Vema, anashuka anaenda kuwaleta. “Walete hapa na uwaache watabiri.” Hawa hapa manabii wote wanakuja, watu waliovalia vizuri, na wenye maadili mazuri, wamebobeza kwenye elimu. Walibobeza kwenye Kiyunani, Kiebrania, na kadhalika. Mnaona?

¹⁶⁰ Wakaja, nao wote wakatabiri. Nao walikuwa na haki ya kutabiri. Wakasema, “Kwea. Kuna nini? Hiyo nchi kule juu ni mali ya Israeli.” Na hiyo ni kweli. “Yoshua alitupa nchi hiyo. Mungu alitupa hiyo, naye Yoshua aliigawanya. Nao watoto wetu wanaishi kwa njaa, na matumbo ya Wafilisti yanashibishwa kwa ngano inayolimwa katika nchi hiyo.”

¹⁶¹ Walijua Neno kabisa, inapofikia kwenye jambo hilo. Bali walikuwa wametenda dhambi na kuipoteza nchi hiyo. Walikuwa wameipoteza. Haikuwa yao hata kidogo, wakati huo, unaona. Lakini, hata hivyo, ukitaka kurudi kwenye msingi, kweli ilikuwa ni yao, na hao manabii walikuwa sahihi.

Wakasema, “Kwea! Bwana yuko pamoja nawe.”

¹⁶² Lakini, unajua, wakati mtu kweli. . . Kama nilivyosema jana usiku kuhusu Yūsufu kuwa ni mtu wa haki. Kulikuwa na kitu ambacho hakikugonga moyoni kwa Yehoshafati. Yeye alikuwa ni mtu mwenye haki. Akasema, “Hivi huna mmoja mwingine?”

163 “Ati mmoja zaidi, na tuna seminari nzima hapa? Walio bora sana tulio nao nchini, manabii wa Kiebrania, nao wanasema kweli kabisa! Angalia jinsi walivyo sahihi sana kwenye Neno. Hilo hapo Neno, lililosema ya kwamba nchi hii ni yetu. Tuna haki ya kwenda kuichukua.”

164 Lakini Yesu alimwambia ibilisi jambo lile lile, na akasema, “Pia imeandikwa.” Hilo ndilo waliloshindwa kuona. Hilo ndilo lililowafanya kutomwamini Yesu. Pia imendikwa, “Bikira atachukua mimba.” Unaona, walishindwa kuona hilo.

165 Kwa hiyo wakati waliposema, “Kweeni mwende huko! Bwana yu pamoja nanyi. Atawapa ushindi kwa sababu hiyo ni mali yetu. Ni—ni katika Jina la Bwana. *Hili* hapa.”

166 Bali haikugonga sawa. Yehoshafati akasema, “Je! una mmoja zaidi ambaye unaweza kumtaka shauri?”

167 Kasema, “Naam, kuna mmoja zaidi, bali ninamchukia. Shirika halitampokea.” A-ha. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Hatutakuwa na uhusiano wowote naye. Yeye ni Mikaya, mwana wa Imla.”

168 Kasema, “Mfalme asiseme hivyo,” kasema Yehoshafati. “Nenda kamlete.”

169 Kwa hiyo basi wakamtuma mtangulizi, kasema, “Mikaya, je! unataka kurudi kwenye ushirika tena? Unaona, sema tu jambo lile lile hao wengine wanalosema. Hii ndiyo nafasi yako sasa. Wewe kubaliana na madhehebu hayo, hao wengine wote, watakurudisha. Unaona? Nawe utakuwa kwenye ushirika na unaweza kufanya mikutano yako kila mahali, kote nchini, basi.”

170 Akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale anayoweka katika kinywa changu.” Tunahitaji akina Mikaya. Akasema, “Nitaona yale Mungu anayosema juu ya jambo hilo, kwanza, kama anataka nirudi huko tena.” Kwa hiyo akasema, “Nipeni usiku wa leo, hebu nione kile Bwana atakachosema.”

171 Ndipo usiku huo bwana akamwonyesha ono. Akalinganisha ono lake na Neno. Hilo lilikuwa liko sawa.

172 Kasema, “Kwea; bali niliwaona Israeli, kama kondoo, wametawanyika, bila mchungaji.”

173 Kwa hiyo basi huyo, kuhani mkuu, ama ninii—ama kiongozi wa Baraza la Ekumenia, akaja na kumpiga kofi mdomoni, na kusema, “Roho wa Mungu alienda wapi wakati aliponiacha?”

Akasema, “Utaona, siku ile wakati ukikaa ndani.”

Kasema, “Alienda wapi?”

174 Naye akasema, akasema, “Nilimwona Mungu ameketi juu ya kiti cha enzi. Niliona jeshi la Mbinguni limekusanyika karibu Naye. Na kukaninii . . .”

175 Nabii wa Mungu! Neno daima humjia nabii. Haidhuru linaonekana lisilopendwa sana na watu jinsi gani, daima liko

hapo. Na sababu ya kujua ndilo, hulitimiza, ya kwamba yale mtu huyo anayonena hutimia. Mungu alisema, basi, hili hulithibitisha. Basi, nabii haimaanishi kunena Neno tu, bali pia ni kutabiri, na ni mfasiri wa Kiungu wa Neno, Neno la Kiungu lililoandikwa. “Neno lilimjia nabii.” Na *huu* ni ufunuo mzima wa Yesu Kristo. *Huu* ndio ufunuo, Biblia. Inamfunua Yesu Kristo. Unaona?

¹⁷⁶ Na sasa, wakati nabii alipojitokeza jukwaani, basi na angetabiri mambo na yangetukia vivyo hivyo hasa, Mungu alisema, “Kumbukeni, Mimi niko pamoja naye basi.” Ndipo wakati alipolifunua Neno, yale huyo nabii mwingine aliyokuwa amesema mbele yake, yakatimia, basi walijua ya kwamba hayo yalikuwa ni kweli. Hiyo ingali ndiyo njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. Yeye kamwe habadilishi njia Yake. Unaona? Kumbuka, yale ma—makundi makubwa walijaribu kubadilisha hilo, bali haikuwezekana.

¹⁷⁷ Huyu hapa mmoja tunayenena habari zake sasa. Nao walikuwa na haki; bali Eliya alikuwa amemwambia Ahabu. Unaona, Israeli walikuwa wamemkubali mtu asiyefaa, ambaye alikuwa amewaundia madhehebu, na alikuwa amelikataa Neno la kweli. Unaona?

¹⁷⁸ Akasema, “Nilimwona Mungu, na baraza likafanywa. Naye akasema, ‘Ni nani tunayeweza kumtuma aende kule chini apate kumdanganya Ahabu?’” Kasema, “Pepo wa uongo akatokea,” labda kutoka kuzimu, “na kusema, ‘Nitashuka niende nikawaingie hao manabii, na kuwafanya watabiri uongo.’”

¹⁷⁹ Manabii wa Kiebrania waliokuwa wakiangalia moja kwa moja kwenye Neno! Mnaona? Ila yale Elisha aliyosema yalikuwa yamewapofusha. Walidhani alikuwa ni mwenda wazimu, pia. Unaona? Lakini wakati Mikaya alipoenda chini ya Roho, aliona yale hasa yule nabii wa kweli aliyokuwa amesema. Hiyo ilikuwa ndiyo nafasi. Ilikuwa ndiyo yenyewe, kufanya hilo. Na hao Waebrania walikuwa sahihi, katika jambo hilo.

¹⁸⁰ Vivyo hivyo hao Waebrania walikuwa sahihi katika yale waliyokuwa wakisema kumhusu Yesu Kristo, mnaona, lakini ilikuwa ni kulingana na upofu wao ambamo ndani yake walikuwa wakitembea. Ilikuwa ni mng’ao wa siku nyingine, si nuru ya siku hiyo. Je! hiyo historia ingeweza kujirudia tena? Biblia inasema hujirudia, unaona. Sasa tunaona ya kwamba kulikuwa na ninii. . .

¹⁸¹ Ilikuwa ni ajabu ya kwamba Mungu alimchagua maskini mtu huyu asiye na elimu, asiye na ushirikiano nao, kuwaonyesha na kuwaletea watu hao Neno; badala ya shule hiyo, ya watu wazuri, wenye maadili, wenye elimu, werevu. Yeye alimchagua Mikaya. Hicho ni kitendawili. A—ha. Hakika kilikuwa ni chenyewe. Na lilitukia vile vile kabisa Mikaya alivyosema

lingetukia, kwa maana alikuwa na Neno la Bwana. Daima imekuwa hivyo. Naam, bwana.

¹⁸² Yohana Mbatizaji alikuwa ni mwingine. Unajua, hatuna taarifa ya kutosha juu ya mahali manabii wanakotoka, na kadhalika, watu wa kiroho. Unaona?

¹⁸³ Mwanadamu humchagua mwanadamu, kama vile walivyomchagua Mathiya, na kuwa huyo apachukue mahali pa Yuda. Hatusikii kabisa juu yake. Mungu alimchagua Paulo. Unaona? Unaona? Hilo lilikuwa ndilo chaguo la Mungu, na chaguo la kanisa. Unaona?

¹⁸⁴ Na ni jambo lile lile, watu waliojazwa na Roho, kwa kawaida ni watu wanaojaribu kutoroka jambo hilo, kulikimbia. Hawataki kufanya jambo hilo. Lakini Mungu hulichukua tu, na kusema, “Nitakuonyesha. Nitakufanya ulifanye.”

¹⁸⁵ Paulo alijaribu kutoroka. Wengine walijaribu kukimbia. Wengi walijaribu kufanya hivyo. Musa alijaribu kulitoroka.

¹⁸⁶ Hatuna taarifa sana ya Yohana. Baba yake alikuwa ni kuhani. Ilikuwa ndiyo desturi katika siku hizo kwa mwana kumfuata baba yake, kazi yake. Lakini wakati Yohana alipozaliwa kwa uzazi wa kuchekesha, wa pekee, wa ajabu sana, wakati alipokuwa amechukuliwa mimba katika tumbo la mamaye. Tunajua hadithi ya akina Zakaria, na jinsi Malaika alivyosema ya kwamba mke wake angepata mimba. Na wakati tunapooni ya kwamba hayo ndiyo yaliyotukia, miezi sita, mtoto hakuwa amecheza.

¹⁸⁷ Naye Mariamu alizuriwa na Gabrieli, kisha akapanda kwenda Uyahudi, kumsalimia, kwa maana Gabrieli alimwambia ya kwamba alikuwa mjamzito. Na alipofika kule, akamwambia, alisema alikuwa amejificha. Na wakati alipokutana na Mariamu, walimpambaja Mariamu na kuanza kumkumbatia, kama wanavyofanya wanawake (wanawake halisi Wakristo, waaminio) akaanza kumkumbatia. Ndipo akasema... aliona alikuwa mkubwa, kuwa mjamzito, naye akasema, “Unajua, Malaika wa Bwana aliniambia nitakuwa mjamzito, pia.” Naye Mariamu, Martha... Samahani.

¹⁸⁸ Elisabeti alisema ya kwamba kwa namna fulani aliingiwa na wasiwasi. Akasema, “Kwa maana, ni miezi sita sasa, wala mtoto hajacheza.” Hilo si jambo la kawaida, unaona. Mtoto huyo kwa kweli, kama tunavyosema, leo, “amekufa,” unaona, ni kama amekufa katika tumbo la mamaye. “Miezi sita.” Lilimsumbua.

¹⁸⁹ Na, mwajua, Yohana alimzidi Yesu umri kwa miezi sita, ambaye alikuwa mtoto wa binamu yake. Mariamu na—na Elisabeti walikuwa binamu. Na wakati tunapooni ya kwamba Elisa-...

¹⁹⁰ Mariamu aliangalia nyuma, uso wa kitoto, na kusema, “Mimi, mimi nitapata Mtoto, pia.”

“Kwa hiyo wewe na Yusufu mmefunga ndoa?”

“La, hatujafunga ndoa.”

“Na ati utapata mtoto?”

¹⁹¹ “Ndiyo, Roho Mtakatifu atanitia uvuli.” Kitendawili! Unaona? “Roho Mtakatifu atanitia uvuli, na Kitu hicho Kitakatifu kitaitwa Mwana wa Mungu.” Kasema, “Gabrieli alikutana na mimi. Na wakati alipokutana nami, alisema nitapata Mwana, nami ‘nitamwita Jina Lake ‘Yesu!’””

¹⁹² Na mara aliposema, “Yesu,” mtoto Yohana akaanza kuruka kwenye tumbo la uzazi la mamaye. Akampokea Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, “Alizaliwa kutoka katika tumbo la mamaye, alikuwa amejazwa Roho Mtakatifu.” Mara ya kwanza Jina hilo lilipotajwa na mdomo wa binadamu, mtoto aliyekufa alifufuka, katika tumbo la uzazi la mama. Linapaswa kufanya kitu gani kwa kanisa lililozaliwa mara ya pili? Hilo Jina, Yesu!

¹⁹³ Kasema, “Mbona unakuja, mbona mama wa Bwana wangu ananijia? Kwa maana mara hizo salamu zilipoyafikia masikio yangu,” yeye alisikia Jina Lake, “mtoto wangu aliruka tumboni, kwa furaha.” Ni jambo la ajabu sana. Ni kitendawili.

¹⁹⁴ Yohana, amekufa, miezi sita katika tumbo la uzazi la mama yake, akafufuka, kwa Jina la Yesu Kristo, mara ya kwanza lilipopata kutajwa na mdomo wa mwanadamu, inaonyesha ya kwamba mtu aliyekufa atafufuka, kwa Jina la Yesu Kristo. Ingali ni kitendawili! “Hakuna jina lingine chini ya Mbingu, walilopewa wanadamu, ambalo unapaswa kuokoka.” Kitendawili! Naam.

¹⁹⁵ Yohana alikuwa ni wa ajabu sana. Ilionekana kana kwamba angaliondoka na kwenda kuchukua kazi ya baba yake, aende kwenye shule yake ambako baba yake alisomea, akiwa Mlawi. Mlawi ndiye tu angaliweza kuwa kwenye ukuhani. Kwa hiyo Yohana alikuwa Mlawi, kwa hiyo hilo, kwa kawaida, lilikuwa—lilikuwa ni desturi kwake kwenda kwenye shule ya baba yake. Lakini Mungu alikuwa na ka—kazi kwa ajili yake; alikuwa amtangaze Masihi.

¹⁹⁶ Kazi yake ilikuwa haina kifani kwa yeye kufuata desturi. Ninatumaini mnasoma sahihi. Kazi yake ilikuwa haina kifani. Asingeweza kwenda kwenye desturi zao na kuchukuana na desturi zao.

¹⁹⁷ Kila mtu angekuwa akisema, “Sasa, hivi hudhani ya kwamba Ndugu Jones, hapa, ndiye mtu hasa anayepaswa kuwa Masihi? Tunajua ya kwamba wewe ndiwe utakayemtangaza. Hivi hudhani yeye ndiye mtu anayefaa?” Ingekuwa ni Mathiya mwingine.

¹⁹⁸ Bali yeye alifanyaje? Alikaa nyikani. Hakuwa na elimu. Yohana, kama vile wengi wetu, leo, asingeweza kuzungumza na kutumia maneno ya sarufi ambayo tungeelezea uvuvio wetu

kwayo, ama mtu, si mimi, labda karibu walio wengi wetu hapa ndani tusingeweza kufanya jambo hilo. Yeye alifanya nini? Ilimbidi kuyaendea maumbile, kuyalinganisha, kuleta jambo analotaka kusema. Unaona? Wakati alipokuwa na jambo la kutangaza, ilimbidi kwenda kwenye maumbile. Angalia, a— alisema, “Enyi uzao wa nyoka,” kile alichokuwa ameona, nyoka jangwani. Aliona hivyo ndivyo walivyokuwa, “Uzao wa nyoka.” Sasa, mtu mwenye elimu angalikuwa na neno fulani lingine, unaona, ambalo angalilitumia badala ya hilo, bali alilielezea kwa “nyoka.”

¹⁹⁹ Kasema, “Msifikiri, mioyoni mwenu, ‘kwa sababu sisi ni washiriki wa *hili*,’ ya kwamba mtamaanisha kitu kwa Mungu, kwa maana Mungu anaweza kwa mawe haya...” Unaona, si kuchukua neno fulani la kitheolojia; hakujua kitu chochote kuhusu seminari. Alikuwa na seminari yake huko nyikani, unaona, mbele za Mungu. Ilikuwa ni ajabu ya kwamba Mungu angechukua mtu kama huyo, ni kitendawili, badala ya watu wote wenye maana, makuhani hao wote wenye elimu waliokuwa shuleni. Ni kitendawili kabisa. Mungu daima hufanya kazi katika vitendawili, kwa maoni yangu.

²⁰⁰ Kuzaliwa na bikira kulikuwa ni kitendawili; bikira kupata mimba, kumzaa Mtoto. Mungu, aliyefanyika mwili; Mungu alibadilisha mwelekeo Wake kutoka—kutoka kwa Roho, akawa Mwanadamu. Mwanadamu anabadilika... Yeye alibadilisha hema Lake, nyumba Yake, na maskani.

²⁰¹ Wakati Yesu alipokuwa amesimama pale, na kwenye pwani za Galilaya, Yohana aliangalia juu na akamwona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka, na Sauti ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.” “Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake,” jambo lile lile; kitenzi kabla ya kielezi, yote sawa, unaona. Unaona? “Huyu ni Mwanangu Mpendwa Wangu ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.” Mungu na mwanadamu wakiwa mmoja, wakiungana pamoja kwa ajili ya ukombozi. Jinsi ambavyo Mungu, aliyefunika anga lote na wakati, angeweza kushuka na kukaa Mwenyewe katika mwili wa Mwanadamu, apate kuonja mauti kwa ajili ya jamii yote ya binadamu! Muumba, akifa, apate kuwaokoa viumbe Wake.

²⁰² Mbingu na nchi zilibusiana, mwanadamu na Mungu wakawa mmoja (mtu anawezaje?) pale, apate kukaa katika mwanadamu na afanye ushirika. Si kitu ila ni Mungu akijishusha, akijaribu kumfikia mtu Wake.

²⁰³ Hapo mwanzo, Yeye alikuwa ndiye Baba. Alikuwa juu ya vitu vyote. Alikuwa peke yake. Aliishi peke yake, Elohimu. Hata wakati aliposhuka mlimani, hata kama mnyama aliugusa mlima huo, hawana budi kufa. Lakini basi, “Alifanyika mwili, nasi tukamshika, tukamshika kwa mikono.” Alifanya jambo hilo

kusudi apate kuimwaga Damu Yake, Damu takatifu; kwa maana sisi tumezaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili. Yeye alizaliwa na bikira. Hakuwa damu ya Myahudi. Wala hakuwa Mmataifa. Alikuwa Mungu, Damu inayoumba. Unaona? Damu ya Myahudi haituokoi. Damu ya Mmataifa haituokoi. “Damu ya Mungu,” Bibla inasema, “inatuokoa.” Yeye alikuwa ni Damu ya Mungu.

²⁰⁴ Watu wengine walisema ya kwamba Yeye alikuwa...ya kwamba, “Mariamu alipata mimba, na ya kwamba hiyo ilikuwa ni ninii...yai lilikuwa ni la Mariamu; seli ya damu ilitoka kwenye jinsia ya mwanamume, ambaye alikuwa ni Mungu.” Hilo ni kosa, pia. Kama ndivyo ilivyo, hebu angalia hapa. Basi, kulishusha hilo yai, ilibidi pawe na namna fulani ya mhemuko. Basi unamfanya Mungu akimfanya nini Mariamu?

²⁰⁵ Yeye aliumba yai na Damu pia. Alikuwa Mungu. Yeye alikuwa ni kiatamizi. Alikuwa tu tumbo la uzazi lililoazimwa. Kama vile kaburi la kuzikiwa lilivyoazimwa. Yeye aliumba vyote. Unaona, hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Alikuwa ni mfano wetu, jinsi inavyotupasa kuwa. Hakumuunga mtu yeyote mkono, bali alifanya yale yaliyompendeza Baba, daima.

²⁰⁶ Na Baba sasa anakaa ndani yetu, kwa mauti Yake. Yeye alilitakasa Kanisa; hiyo ni kweli kabisa, Kanisa hili, lile saf... lisilo safi, chafu. Mungu akijidhili, kutoka kwenye Nguzo ya Moto; akashuka apate kufanyika mwanadamu; na halafu Roho Mtakatifu moja kwa moja ndani yetu. Hivi huoni ni kitu gani? Mungu yeye yule akishuka wakati wote, sasa. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi; Mungu ndani yetu. Unaona? Kama vile, mawazo ya Mungu; Neno la Mungu, na dhihirisho la Neno.

²⁰⁷ Ni jambo lile lile tu, tangu mwanzo, Mungu akiwaza; Baba, Yeye alikuwa; Mwana, alikuwa; Mwokozi, alikuwa; alikuwa Mponyaji.

²⁰⁸ Maneno hayo yalinenwa, nayo yalidhihirishwa, “Bikira atachukua mimba na atamzaa Mwana; ataitwa Jina Lake Immanueli, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele,” na ikawa hivyo!

²⁰⁹ Na kutoka hapo, ikatokea, “Apate kuwazaa wana wengi kwa Mungu.” Jambo hilo lote ni Mungu, aliyefunuliwa! Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; Mungu ndani yetu. Kitendawili, kweli, ya kwamba Mungu angeishi ndani ya mwanadamu, Mwenyewe. Hakika.

²¹⁰ Ilibidi afanyike huyo, apate kufa, apate kuridhisha sheria Zake Mwenyewe za haki. Alibashiri, na kusema, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Naye ilimbidi kutimiza, hakukuwa na mtu mwingine angaliweza kufanya jambo hilo ila Yeye Mwenyewe. Kama—kama Yeye...

²¹¹ Leo, katika siku hii, ninapenda kuleta jambo hili, la—la Uungu wa Yesu Kristo, kwa sababu watu hujaribu kumfanya

Yeye nabii. Sasa kama ikitokea kuna Mkristo wa Kisayansi anayeketi hapa, siwaudhi; natumaini siwaudhi.

212 Lakini tunatilia mkazo sana madhihirisho ya ishara. Sisi Wapentekoste tunaweka ushuhuda wetu juu ya kunena kwa lugha, na jinsi ambavyo tumepumbazwa vibaya na jambo hilo. Na ni wangapi wao wanaosema, “Tunda la Roho ndilo thibitisho,” jinsi ambavyo mnapumbazwa sana na hilo. La, bwana. Kama ukizungumza kuhusu kunena kwa lugha kwamba ni thibitisho la Roho Mtakatifu. . . Ambapo, ninaamini Roho Mtakatifu hunena kwa lugha. Msinieleva vibaya. Naam, bali mnasema, “Mtu akinena kwa lugha, ana Roho Mtakatifu.” Tuliaini hilo kwa kitambo kidogo, bali tulikuta kwamba ilikuwa si kweli.

213 Luther alisema, “Wale waliosema ya kwamba wanaamini.” Tulikuta kwamba hiyo ilikuwa si kweli. Wesley akasema, “Wale waliotakaswa na wakapiga makelele.” Tulikuta kwamba hiyo haikuwa ni kweli. Pentekoste walisema, “Wale walionena kwa lugha.” Tulikuta kwamba hiyo ilikuwa si kweli. Wakristo wa Kisayansi walisema, “Tunda la Roho ndilo thibitisho.” Tunakuta kwamba hiyo haikuwa ni kweli.

214 Nimewaona wachawi na walozi wakinywa damu kutoka katika fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kunena kwa lugha; na kuweka penseli juu ya meza na inaandika kwa lugha zisizojulikana, na wanaifasiri lugha hiyo. Unaona? Sasa, usiniambie juu ya jambo hilo; mama yangu ni Mhindi nusu, unaona, nami ni—nami ninajua. Nimeona jambo hilo na kulishughulikia.

215 Hata hivyo, Mungu hunena kwa lugha, bali hilo si thibitisho lisilokosea ya kwamba una Roho Mtakatifu. La hashi. Hapana, kweli. Mkristo si . . . Hebu ni ninii . . .

216 Mungu anisamehe kwa kufanya jambo hili. Nitamweka Yesu kwenye mashtaka kwa ajili yenu, kwa muda kidogo tu, kama mtanisamehe. Je! nina wakati wa kufanya hilo? Hebu na tuone, hebu kidogo. [Ndugu mmoja anasema, “Naam, chukua wakati wako.”—Mh.] Hebu iweni tu. . . Naam, ni—nimepita wakati kwa dakika kumi, bali nitaharakisha na niruke baadhi ya haya, mnaona. [Ndugu mwingine anasema, “Hawakuweka wakati wowote.”] Hebu na tujaribu jambo hili kwa dakika moja tu, ndugu.

217 Sasa, Baba wa Mbinguni, nisamehe kwa ajili ya jambo hili. Sitaki kulinena, bali ni ili kwamba watu wajue.

218 Nitachukua ya kwamba ninampinga Yesu, asubuhi ya leo, nami nitasema ninyi ni kundi la Wayahudi, na kwamba Yesu alitokea tu hapa Bakersfield. “Hebu niwaite ninyi watu pamoja na kuzungumza nanyi kuhusu matunda ya Roho.” Wanaamini jambo hilo, pia.

219 Tunda la Roho ni nini? Upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, wema. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tunda la Roho, watu wengi wanategemea hilo.

220 Mara nyingine huyo ni ibilisi. Anaweza kuiga jambo hilo, kikamilifu; yeye haki-...anaweza kuiga kunena kwa lugha, kikamilifu; fasiri yake, kikamilifu. Yoyote ya karama hizo, anaweza kuiga.

221 Angalia, “Ninaenda,” huyo hapo kuhani, “nitazungumza na ninyi nyote.” Sasa ninampinga Yesu, kwa dakika moja tu. Nimemwomba Mungu anisamehe, ili kwamba tu niweze kuwaonyesha yale ninayomaanisha, kuleta ukweli fulani. Unaona? Nitasema...

222 “Waungwana, niko hapa kwa niaba ya kanisa lenu, asubuhi ya leo. Ninawazungumzia ninyi nyote. Sasa, kuna jamaa kijana fulani hapa mjini, jina Lake Yesu, wa Nazareti. Ana fundisho la kigeni. Sisi tunawajua makuhani wetu. Sasa itatulazimu kuamua jambo hili kwa tunda la Roho. Huyu, kuhani wenu, babu wa babu wa babu wa babu yake alikuwa ni kuhani. Aliachana na maisha yake yote ya ujana, mambo yale yote ninyi mliyofurahia wakati mkiwa vijana. Aliyaacha hayo, kusudi awe kuhani kwa Mungu. Alifanya nini apate jambo hili? Alisoma, alifanya yote aliyoweza kufanya, apate kuwa mtu anayestahili.

223 “Ni nani aliyewafariji wakati baba na mama walipokuwa wakizozana, nao walikuwa wakitaka kutengana? Ni nani aliyewasihi baba na mama, akamkumbatia mmoja, kisha huyo mwingine, na akawapatanisha? Maskini kuhani wenu mwaminifu aliyepo pale. Maskini kuhani wenu mzee mwaminifu alisoma torati za Yehova mpaka akajua barabara, barabara, barabara. Alipitia katika kila seminari. Yeye ana Shahada ya juu sana ya Theolojia. Shahada ya Kwanza, anayo. Ana D.D., L.L., Ph.D. Anajua kile hasa anachozungumza habari zake. Alizisomea hizo, wakati ninyi watu mlipokuwa mkizurura. Alizisomea, kwa sababu yeye ni kiongozi wenu.”

224 Yote hayo yanaleta maana, ndugu zangu, kama unazungumza kisaikolojia juu ya jambo hilo. Yote yanaleta maana.

225 “Huyu Yesu wa Nazareti alitoka kwenye shule gani? Hajawahi kamwe kwenda shule hata siku moja, kadiri tujuavyo sisi. Alitoka wapi? Hakuna ajuaye; huyu hapa anakuja huku. Hebu mwangalie maskini kuhani wako mzee mwema. Wakati baba yako alipopungukiwa na pesa wakati huo, hakuwa na pesa, je! alimwendea nani? Mtu aliyekuwa na tunda la Roho, maskini kuhani wako mzee mwema ambaye alimkopesha hizo fedha ampe zaka mpaka mazao yake yatakapoingia ndani.

226 “Ni nani aliyekufariji wakati mama yako alipokuwa katika utungu wa kuzaa?” Samahani, akina dada. “Nao walidhani atakufa. Ni nani aliyeshikilia mikono yake juu yake, na

kuomba, wakati ulipokuwa ukizaliwa humu ulimwenguni? Maskini kuhani wenu mwema. Ni nani aliyekuinoa juu kwa Yehova, na akakutahiri, na akakushika na kukufanya uninii... na akakukabidhi kwa Yehova? Maskini huyo kuhani mwema.

227 “Basi hebu angalia kile huyu Yesu wa Nazareti alichofanya, hivi majuzi. Angewahi kufanya nini kwa suala la tunda la Roho?”

228 “Sasa, wengi wenu ni wafanyabiashara, mna—mna biashara hapa. Ninyi, ninyi ni wafanyabiashara, na—na kadhalika. Yehova anahitaji mwana-kondoo kwa ajili ya dhambi zenu. Ninyi hamfugi wana-kondoo. Kwa hiyo maskini hawa makuhani wema wamefanya nini, ili kwamba nafsi zenu zisipotee? Waliwaagiza wauzaji waende kule uani, wakajenge vizimba vidogo, na kuweka wana-kondoo humo; mpate kuchukua mapato yenu, ambavyo ndivyo mngepaswa kufanya; hamfugi wana-kondoo, bali mlipata kitu kingine, kuendeleza uchumi wetu. Nao wanacheza... wakatengeneza mahali ili kwamba ninyi, mtakapolemewa na dhambi, na mnataka msamaha wa dhambi zenu. Maskini kuhani huyu mwema alikuwa na mahali ambapo mngaliweza kwenda na kununua mwana-kondoo. Mungu hakutaka fedha zenu; Yeye alisema, ‘mwana-kondoo,’ nanyi mliondoka mkaenda na kununua mwana-kondoo!”

229 “Huyu Yesu wa Nazareti alifanya nini? Alikuwa na akatupilia vitu hivyo nje, na kuvimwaga, na akawaambia eti wao walikuwa ni ‘pango la wanyang’anyi.’ Hakuna matunda mengi ya Roho hapo, sivyo? Maskini kuhani wenu mwema kamwe hapandishi hasira. Jamaa huyu alisokota kamba, na akazipindua meza, na kuwafukuza watoke nje, na kuwaangalia kwa hasira. Hilo halikuwa ni tunda la Roho. Maskini kuhani wenu mwema! Ni nani atakayeyakariri maneno ya mwisho juu yako? Maskini kuhani wako mwema. Ni nani atakayeruhusu, kuikabidhi roho yako kwa Mungu? Maskini huyo kuhani mwema. Unaona, tunda la Roho lilifanya jambo hilo. Na huyo Jamaa hakuwa na hata moja la hayo!”

230 Sasa unasema, “Ndugu Branham!” Nginghubiri somo nzima juu ya hili, bali sitahubiri.

231 Tunda la Roho ni nini? Dhihirisho la Neno lililoahidiwa. Laiti tu wangelisimama kuangalia, Yeye hakuwa na mambo haya waliyokuwa nayo, tunda la Roho, wala chochote kile. Lakini Neno lililoahidiwa siku hiyo alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe, hiyo ilikuwa ndiyo Nuru ya wakati huo hasa. Hiyo ilikuwa ndiyo Yenye, mnaona.

232 Haidhuru ni kiasi gani cha elimu, na ni mtu mwema jinsi gani, unanena kwa lugha kiasi gani, u mwema vipi, u mwenye utu wema kiasi gani, na chochote ulicho; isipokuwa ulikubali Neno hilo la saa hiyo, wakati limedhihirishwa mbele zako, uko katika hatari ile ile.

233 Hilo linaweza kusikika kuwa ni kali, simaanishi iwe jinsi hiyo, bali ni Kweli. Ninii tu, liaminini tu, mnaona. Vema. Sasa Mungu anisamehe. Mnaona ninalomaanisha?

234 Ni nani aliyekuwa na tunda la Roho? Yesu! Yeye alisema, “Mwayachunguza Maandiko. Mnadhani hayo...Ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Yananishuhudia Mimi. Yanawambia kwamba Mimi ni Nani.” Yeye kamwe hakutokea na kusema kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Yeye hakuwaambia. Pia kusudi la kulifanya kusanyiko Lake lenye ukubwa huo...Yeye alisema, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake,” kama nilivyosema jana usiku, “hamna Uzima.”

235 Mbona, jamani, kusanyiko hilo lilisema, “Jamaa huyo ana kichaa. Madaktari na sayansi wangeninii...Vema, mtu huyo anajaribu kutufanya sisi kuwa wala watu.” Hakulielezea kamwe. Ulikuwa ni wakati wa wao kumkataa.

236 Ndipo alikuwa na kundi la wahubiri wakimganda, waaminio wakwamia mpaka. Yeye alisema, “Vema, ninyi mtasema nini mtakaponiona Mimi nikipaa juu kwenda nilikotoka?”

237 “Ati ulikotoka? Vema, sisi tumeona kitanda kidogo ulimozaliwa, mji ulimozaliwa. Tumevua samaki pamoja na Wewe, hapa nje vilimani. Wewe, tunatembea pamoja na Wewe, tunazungumza na Wewe, Nawe unatoka...? Loo, jamani, sasa tunajua Wewe una kichaa.”

238 Lakini imani halisi, ya kweli haitikisiki. Hao wanafunzi wasingeweza kuelezea jambo Hilo, bali walijua ndio hilo hapo lenyewe. Unaona? Haina budi kuwa ni kitu ambacho Mungu alipanda, ilibidi kiwe kilikuwa ni mawazo Yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati alipowakusudia wote waliokombolewa. Waefeso 1:1-5, Yeye aliandaa kitu hicho chote kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, mawazo Yake, na hili ni sifa za mawazo Yake.

239 Mwangelie Yuda akiwa amesimama pale, kama kasisi hapa juu, “Naam, akitembea katika Nuru,” alikuwa na nguvu za kuwaponya wagonjwa. Mathayo 10 inathibitisha jambo hilo. Yeye aliwatuma huko, nao walirudi wakifurahi, na pepo walikuwa wakiwatii. Yuda akiwa pamoja nao! Hiyo ni kweli. Yeye alisema, “Msifurahi ya kwamba pepo wanawatii; bali majina yenu yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.” Yuda alikuwa pamoja nao. Lakini wakati ilipofikia kulichukua Neno lote la Mungu, alilikataa.

240 Vivyo hivyo na watu, leo! Unaona? Yesu alisema, “Mtu ataishi kwa kila Neno,” si Neno moja ama mawili tu. Kila Neno!

241 Unasema, “Vema, Ndugu Branham, ninaweza kuamini sehemu ya Hilo. Na siwezi kuamini...”

242 Basi una yule mfasiri ambaye Hawa alikuwa naye. Aha. Alichukua kila sehemu Yake, akalifasiri vizuri, ila fungu

moja dogo la maneno. Inapaswa kuwa ni kila sehemu Yake. Kama Biblia inalisema hivyo, si ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote. Ni vile Biblia ilivyosema. Na kama Mungu alisababisha magonjwa haya yote ya moyo na huzuni, na vifo vya watoto wachanga, na vilio, na vita, na kadhalika, kwa sababu fungu moja la Neno Lake lilitiliwa shaka, je! Yeye atakuchukua kwa lolote pungufu la Hilo? Wazia jambo hilo.

²⁴³ Yeye habadiliki. Uamuzi Wake wa kwanza hauna budi kudumu uamuzi huo huo. Hiyo ndiyo sababu Yeye hushughulika na mtu mmoja binafsi, sio na kundi. Mmoja! Yeye hawezi kubadilisha hilo. Vema, nina mengi sana ya kusema hapa, bali nitaninii. . .

²⁴⁴ Kifo cha Yesu kilikuwa ni jambo la ajabu sana. Kilikuwa ni kitendawili. Kule kufufuka kulikuwa ni kitendawili. Tunaamini jambo hilo. Kila mtu anajua ya kwamba kule kufufuka kulikuwa ni kitendawili, ya kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu.

²⁴⁵ Kuzaliwa upya ni kitendawili. Hiyo ni kweli, kunaweza kubadilisha utu wa mtu! Tungeweza kuhubiri mahubiri papa hapa katika muda mfupi, unaona, jinsi ambavyo kitendawili, kumchukua mtu ambaye haamini, asiyeamini, hana uhusiano wowote na jambo Hilo, na mara moja kumbadilisha kutoka kuwa kafiri akawa mtakatifu, malaya akawa dada. Ni kitendawili. Hakuna mtu anayeweza kumpa dawa, wala kumdunga sindano, wala dozi ya dawa, wala chochote kile; Hilo linahitaji mkono wa Mwenyezi Mungu, na huo pekee, kumbadilisha mwanadamu. Vema, ni kitendawili, wakati mtu anapozaliwa mara ya pili, hilo ni kweli, ni kitendawili tena.

²⁴⁶ Ilikuwa ni kitendawili wakati Mungu alipowachagua wavuvi wajinga mia moja na ishirini, kupeleka habari, Injili siku ile ya Pentekoste, kote ulimwenguni, badala ya lile—lile Baraza kuu la Wazee lililokuwa limefunzwa kwa kusudi hilo, wale waliokuwa wamefunzwa na wakingojea, na wakangojea jambo hilo kutukia. Ndipo Mungu akajifunua Mwenyewe kwa kundi la wavuvi ambao hata wasingeweza kuandika jina lao wenyewe kwenye kipande cha karatasi. Ni kitendawili, kwamba Mungu alichagua watu kama hao, badala ya kuchukua lile—lile Baraza la Ekumeni la siku hiyo, kufanya jambo hilo.

²⁴⁷ Litafanyika jambo lile lile leo. “Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

²⁴⁸ Maono ya manabii daima yamekuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo watu hao, kwa uvuvio, wangeweza kutabiri mambo ambayo hayakosei kamwe. Hicho ni kitendawili, jinsi ambavyo kitu fulani zaidi ya mawazo ya kibinadamu, ambacho huwezi kufahamu. Ziko mbili, dhamira na dhamira ya ndani; kwamba Mungu huingia katika dhamira ya ndani, ambayo ndiyo halisi, na anaona mambo yajayo, anamchukua na anaona mambo yaliyokuwa huko nyuma kabisa katika wakati mwingine,

anamleta kwenye wakati uliopo na kumwambia habari za usoni, wala halikosei, wakati wowote. Kitendawili, kweli! Haiaminiki, bali ni kweli. Hutukia vivyo hivyo hasa. Yale tuliyomwona akifanya jana usiku yalikuwa ni kitendawili, hayaaminiki kwa macho ya kibinadamu. Hatuwezi kuyaelezea.

²⁴⁹ Kanisa fulani la Kibaptisti ambako maskini familia yangu ndogo ilihudhuria, hivi majuzi, nao walikuwa wamehudhuria mkutano huko Tucson. Mchungaji aliamka, bila kujua ya kwamba yule mvulana anayeambatana na binti yangu ni mshirika kule. Naye akasema, “Mwajua, nilisikia tu, baba yake Ndugu Branham na mama yake walisafiri katika sa—sarakasi.” Tena akasema, “Walikuwa ni wachawi, na huo ni ujanja mdogo anaofanya.” Unaona? Nafikiri ni ujanja fulani unaowaponya wagonjwa? Nina shaka kama baba yangu na mama yangu walipata kuona sarakasi. Hawakuwahi kuona motokaa mpaka niliponunua moja. Mnaona? Hawakujua kamwe kitu chochote juu yake.

²⁵⁰ Lakini, unaona, ibilisi daima ana jambo la kusema. Walimwambia Yesu, “Wanafanya jambo hili kwa Beelzebuli.” Ilibidi wajibu jambo fulani kwa kusanyiko lao. Kwa nini hawayachunguzi Maandiko na kuona hili lilibashiriwa kwa siku ya leo. Ni Yesu Kristo ye—yeye yule, jana, kama alivyokuwa jana ndivyo alivyo leo, na atakuwa hivyo milele. Lakini jambo hilo ndivyo lilivyo, mnaona, hiyo ni ninii tu—jinsi ambavyo wanajaribu kulitenda jambo hilo, wale Wapentekoste wasio na elimu, hayo maono ya nabii. Yesu kuwa hai leo, baada ya miaka elfu mbili, ni kitendawili, pia. Kweli ni kitendawili.

²⁵¹ Sasa sina budi kufunga, maana muda unaenda. Je! mnaamini katika kitendawili? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika.

²⁵² Hebu niseme jambo hili. Wakati mmoja rafiki yangu mzee mwuza madawa, mzee mwema, alisema, “Ndugu Branham, nitakwambia jambo fulani.” Akasema, “Ni—ninajua huduma yako,” basi akasema, “Ni—nitakwambia.” Kasema, “Huenda likasikika kama haliaminiki. Lakini,” akasema, “Sijawaambia watu, kwa maana wasingeliamini. Lakini,” akasema, “nitakwambia.”

Nikasema, “Endelea.”

²⁵³ Akasema, “Papa hapa kwenye duka lili hili la madawa,” akasema, “wakati ule wa kuzorota kwa uchumi, nilikuwa nimeketi hapa. Mvulana wangu, ambaye sasa ameo na anauza dawa kwenye duka la madawa katika mji mwingine,” kasema, “alikuwa akiwangojea wateja.” Ndipo kasema, “Watu walikuwa...” Kasema, “Iliwabidi waende kwenye... Unakumbuka wakati mtu ilikubidi kwenda na kupata oda kutoka wilayani, ukanunue dawa yako. Chochote kilichokubidi kupata, ulipaswa kwenda kuchukua oda kwa ajili ya kitu hicho.”

Alisema kwamba aliona mume na mke wakijikokota kuingia mlangoni, naye akasema aliangalia. “Maskini, mama mdogo, mja mzito, alisimama kwa shida; kijana mwanamke, alikuwa tu akitembea.”

²⁵⁴ Naye akasema, “Kijana mwanamume huyo alimwendea mwanangu, na kusema, ‘Nina oda hapa kwa ajili ya ninii... Daktari alinituma hapa kupata hiyo oda, hasa, kutoka kwa ajenti wa wilaya hapa, ku—kununua dawa. Mke wangu anaihitaji sana.’ Kisha akasema, ‘Hawezi kustahimili zaidi,’ kasema, ‘anaumwa sana. Daktari aliniambia, “Kainunue sasa hivi na umpe.”’ Kasema, ‘Sijui kama ningeweza kupata hiyo dawa, na nimpe dawa hiyo, naye angeweza kuketi chini hapa?’ Ndipo akasema, ‘Itanichukua saa mbili ama tatu, kusimama kwenye mstari huo, kabla sijapata oda yangu kwa dawa hiyo.’ Kasema, ‘Sijui kama ungeweza kunipa hiyo dawa sasa?’

²⁵⁵ “Kijana huyo akasema, ‘Bwana, ningependa kufanya hivyo.’ Kasema, ‘Siwezi kufanya jambo hilo,’ akasema, ‘kwa sababu jambo lenyewe ni kwamba tuna she—sheria hapa, ya kwamba, sisi, ni utaratibu wa kulipa pesa taslimu na kuchukua.’ Akasema, ‘Inabidi tuutekeleze.’”

²⁵⁶ Naye akasema alikuwa ameketi nyuma kule, akisoma gazeti, mtu mzee. Akasema, “‘Ngoja kidogo, mwanangu.’ Akamwangalia maskini mwanamke huyo amejishikilia tu namna hiyo.” Na kwa hiyo akasema, “‘Nenda kajaze oda hiyo.’ Akasema, ‘Uniletee hapa.’”

²⁵⁷ Kasema alichukua maagizo hayo ambayo daktari alikuwa amempa, akaondoka akaenda pale na akayajaza. Kasema, “Nikaajaza, na kuwazia, ‘kama hatailipa kabisa, ni sawa, haiteti tofauti yoyote.’”

²⁵⁸ Kasema, “Nilienda mahali yule mama alipokuwa. Nikaichukua, nipate kumpa mkononi mwake.” Ndipo kasema, “Nilipoiweka mkononi mwa mwanamke huyo,” kasema, “nikaangalia juu.” Kasema, “Ndugu Branham, sijui kama utaamini jambo hili ama hutaamini.” Kasema, “Niliweka kwenye mikono ya Bwana Yesu.” Kasema, “Nilimwona amesimama pale, akiniangalia, na Damu ikitiririka usoni Mwake, na makovu kwenye kichwa Chake.” Kisha akasema, “Nilifunga macho yangu, namna *hiyo*, kwa namna fulani nikayumbayumba. Ndipo nikamsikia mume wake akisema, ‘Uko sawa, Daktari?’” Naye akasema, “‘Ndiyo.’” Kasema, “Nikaangalia nyuma, na yule mwanawake alikuwa ameishika ile oda.”

Kasema, “Je! unaamini jambo hilo?”

²⁵⁹ Nikasema, “Hakika, ninaliamini. ‘Kadiri mlivyowatendea walio wadogo sana wa hawa watoto Wangu, mmenitendea Mimi.’” Kitendawili, hasa!

²⁶⁰ Wengi wenu ndugu hapa mmesoma maandiko ya Mtakatifu... ya watakatifu wa siku za mwanzoni, jinsi ambavyo Bwana alivyowashughulikia, kitendawili, jinsi ambavyo mambo yalitendeka. Tunaamini katika kitendawili. Moja ya...

²⁶¹ Mtakatifu Martin alikuwa ndiye niliyekuwa nikijaribu kumwazia. Unaona, yeye alikuwa askari, na huko Ufaransa lilitolewa agizo kwamba anapaswa kufuata kazi ya baba yake. Lakini daima kwa namna fulani aliamini. Mama yake alikuwa ni mwaminio. Na siku moja yenye baridi... Yeye alikuwa ni mtu mnyenyekevu sana, na daima walikuwa na mtu wa kupiga buti zake rangi, na kumfanya aonekane nadhifu, kama askari apaswavyo kuwa. Yeye alizipiga buti za mtumishi wake rangi. Yeye hakufuata desturi zao na mila za ukoo wao. Alifikiri wanadamu waliumbwa wakiwa sawa.

²⁶² Kwa hiyo siku moja yenye baridi, alikuwa amesimama karibu na lango la mji wa Toras, wakati alipokuwa akiingia, na akasema hapo alilala maskini mzee mwombaji barabarani. Mmekwisha kusoma hayo, hapana shaka, mara nyingi. Palikuwa na mwombaji amelala barabarani, akifa kwa baridi kali, kipupwe chenye baridi kwelikweli. Alikuwa akiwaomba watu, "Njoni! Yu—yupo mtu anayeweza kunipa joho? Nitakufa kwa baridi, usiku huu. Siwezi kulala kwenye sakafu namna hii. Yupo mtu anayeweza kunipa koti?" Hakuna mtu. Akasema, "Tafadhali, mtu fulani anihurumie; maskini mzee, ninakufa. Nimeutumikia muda wangu. Nimefanya vizuri nilivyoweza. Msiache nife. Ninakufa kwa baridi. Mtu fulani na anifunike, je, mtanifunika?"

²⁶³ Na kwa hiyo akasimama nyuma tu, Mtakatifu Martin, akiangalia. Yeye hakuwa mwaminio, hakuwa Mkristo wakati huo, hakuwa ameukubali. Alisimama tu na kuangalia. Hakuna mtu aliyefanya hivyo, wakati umati wa watu ulipopita hapo karibu, baadhi yao wanajiweza sana kumsaidia. Yeye alikuwa na koti moja tu, na hilo lilikuwa ni koti lake la kijeshi. Alivuta upanga wake akalikata, akaligawanya nusu vipande viwili, akamfunika maskini yule mwombaji nacho, kisha akaenda zake.

²⁶⁴ Watu walimcheka akishuka kwenda barabarani, kipande kimoja cha koti kimening'inia mwilini mwake. "Ni askari wa kuchekesha jinsi gani," walisema alichekesha, wakamdhihaki.

²⁶⁵ Usiku huo aliamshwa, katika usingizi wake. Aliangalia, akiwa amesimama karibu na kitanda chake, na pale alisimama Yesu amejifunika kile kipande cha koti ambacho alikuwa amemfunika nacho yule mwombaji. Ndipo akajua, "Kadiri mlivyowatendea walio wadogo sana wa hawa watoto Wangu."

²⁶⁶ Ilikuwa ni kitendawili, wito wake. Yeye alikuwa ni yule—alikuwa ni mjumbe wa wakati huo. Aliyatetea Maandiko, dhidi ya uovu wote wa ukatoliki katika siku hiyo. Mungu alimchagua, Naye alimruhusu kumwona Kristo, kwa kitendawili.

²⁶⁷ Ndugu, tunaweza kuona kitendawili baada ya kitendawili. Kile kitendawili kikubwa kinakuja mbele zetu, “Wakati Baragumu ya Bwana itakapolia, na hakutakuwako na wakati baada ya hiyo; na ile asubuhi ipambazuke Milele nyeupe isiyo na mawingu.” Wakati ufufuo utakapokuja, nasi tunanyakuliwa pamoja, kumlaki Yeye hewani, hicho kitakuwa ndicho kitendawili cha mwisho, tutakapokwenda kuwa pamoja Naye. Mpaka wakati huo, na tuwe watumishi waaminifu kwa Neno la Mungu, ambalo ni Kristo.

Twaweza kuomba?

²⁶⁸ Baba wa Mbinguni, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa Damu inayotufanya ndugu. Tunakushukuru kwa ajili ya Mwana wa Mungu ambaye aliutoa uhai Wake, tupate kuwa mmoja pamoja na Yeye katika Ufalme huu mkuu juu ya nchi, Ufalme wa Mbinguni utakaoanzishwa. “Tunaitazamia hiyo siku nzuri ya ule Utawala wa Miaka Elfu, wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja na kumnyakua Bibi-arusi Wake anayengojea kwenda naye,” ule Mti mdogo wa Bibi-arusi. Yeye ni ule Mti uliokuwa katika bustani ya Edeni; kile Chakula cha Uzima. Vivyo hivyo maskini mke Wake ni mti, Mti wa Bibi-arusi wa siku za mwisho. Ambapo, kila kitu kimejaribu kuleta, bali zile nguvu kuu za Mungu zinayakata matawi, kusudi tunda lipate kukomaa. Tujalie, Bwana, kusudi tuweze kujumuishwa mle. Tupe sisi Uzima wa Milele.

²⁶⁹ Tuna jambo hili moja shirika, wakati tukiwa hapa katika mji huu, tunaamni Neno la Mungu. Tunamwamini Yesu Kristo. Tunaamini ya kwamba Yeye si mfu, bali yu hai. Na Maneno Yake, ile ahadi kwa ajili ya saa hii, sasa inadhihirishwa. Hizi ndizo saa za mwisho. Hii ndiyo ishara ya mwisho. Kuja kwa Bwan- . . . Yule Mwana aliyeahidiwa yuko karibu.

²⁷⁰ Tunaona ulimwengu, kijiografia. Tunaona zile ishara; matetemeko ya nchi mahali mahali, mataifa dhidi ya mataifa. Tunaona mambo yote yaliyobashiriwa. Tunaona vitu vya kutisha angani, mioyo ya watu ikizimia; visahani virukavyo, na kadhalika, wasivyoweza kuelezea, hukumu ya kuchunguzwa ikija duniani. Tunaona makombora ya atomiki yakining’inia huko ng’ambo, kila mahali, na yale makombora makubwa yanaweza kusababisha maangamizi mabaya sana katika saa moja. Tunaona gesi zikining’inia huko juu yetu, ambazo zingenyeshwa mioto mikubwa mno huku chini, kutoka angani, na kuiangamiza dunia.

²⁷¹ Lakini tunamwona Yesu, pia, ambaye alitoa ahadi! Na kama ilivyosemwa, “Yesu yuyu huyu, aliyetwaliwa juu toka kwenu, atarudi tena jinsi mlivyomwona akienda Mbinguni.” Tunaitazamia hiyo Siku nzuri kuja.

²⁷² Mioyo yetu, wengi wetu hapa, Bwana, kwani tangu tulipokuwa wavulana wadogo, tumefanya kila jitihada

tuliyojua, kukutumikia. Bwana, usiache macho yetu yapofushwe yasiione saa hii. Yafungue macho yangu, Bwana, nipate kuona kila ahadi. Jalia niweze kuiitikia kwa “amina,” kwamba ni kweli, kila kitu ambacho Mungu ameahidi. Tujalie, Bwana. Tupe mkutano mkuu.

²⁷³ Wabariki hawa, ndugu zangu na dada, hapa. Baadhi ya maskini wanawake hawa wanaosimama hapa, wenye mvi, waliotumika katika—katika kuwatunza mabwana zao, wakati wakifanya kazi huko makondeni. Na, Mungu, utawapa thawabu, hao wanaume ambao wamepigana vita wapate kushinda tuzo, na wakaabiri katika bahari zilizojaa damu. Tunapoketi hapa asubuhi ya leo, kuizunguka meza hii, tukiangaliana, na nywele zetu zinaingia mvi, nasi tumepigana muda mrefu, na huenda tusikutane kwenye kiamshakinywa kingine. Hatujui.

²⁷⁴ Huenda Kuja kwa Bwana kukawa ni leo, huenda kukawa ni kesho, huenda kukawa ni mwaka ujao. Hatujui itakuwa ni lini. Bali kuna jambo moja la hakika, tumeahidiwa ya kwamba tutakutana kwenye Chakula cha Jioni hewani, naye Mfalme atatoka na kupangusa machozi yote machoni mwetu, na kusema, “Msifadhaike; yote yamekwisha sasa. Ingieni katika raha za Bwana, ambazo mmeandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati tulipochaguliwa kuwa wana wa Mungu, kwa Yesu Kristo. Ee Baba, Mungu, tujalie jambo hili.

²⁷⁵ Jalia mioyo yetu idunde kama moyo mmoja. Na kama nilivyosema muda mfupi uliopita, kwa maskini yule bwana na mkewe waliokuwa karibu ya kutengana... Mungu, tunapoachana hapa, tuliona hili jambo moja tulilo nalo shirika. Methodist, Baptist, United, Waassemblies, Kanisa la Mungu, sote tuna kitu kimoja shirika, Yesu Kristo. Hatuwezi kukutana kama madhehebu, na kuzozania hizo kanuni za imani na kadhalika za kanisa. Bali kama ndugu, tunaweza kukutana chini ya Damu ya Mwokozi wetu, Yesu Kristo, na hapo tuna mambo shirika. Na juu ya msimamo huu wa pamoja, Bwana, ninakuja kukutana na ndugu zangu, watu wa Imani moja, ya thamani. Tujalie sisi, pamoja, katika juma hili lijalo, tufanye kazi kwa juhudi zote, tupate kuona utukufu wa Mungu ukirudishwa kanisani tena. Tunakabidhi kila kitu Kwako, pamoja na sisi wenyewe. Katika Jina la Yesu, bariki jitihada zetu. Amina.

²⁷⁶ Awabariki, ndugu zangu. Ndugu Roy, je! ulikuwa na neno la kusema? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁷⁷ Jinsi Neno lisivyoweza kukosea! Yesu alikuwa Neno. Tutakubaliana juu ya hilo. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wakati wazazi Wake walipokuwa wamemsahau, na wakamwacha kule kwenye karamu, nao walikuwa wameenda safari ya siku tatu wala wasingempata, ndipo wakarudi. Tulimkuta hekaluni, akijadiliana na makuhani, nao walishangazwa na Mtoto huyu. Hatuna taarifa Yake ya kwenda

shuleni. Lakini, kumbuka, Yeye alikuwa ni Mvulana tu, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, kimo *hiki*. Na hebu angalia tamshi la mama Yake.

²⁷⁸ Sasa, si kuwadharau ninyi Wakatoliki, kama yupo yeyote hapa, anayemwita “mama ya Mungu.” Anawezaje kuwa mama ya Mungu? Unaona, alikuwa ni kiatamia ambacho Mungu alitumia, si ma-... Hebu mwangalie, kama alikuwa ni mama wa Mungu, kwa kweli huyo mama alikuwa na hekima nyingi zaidi kuliko Yeye, angalia, wakati yeye ni mama, alimpa Yeye uhai, alimpa Mungu uhai. Unaona?

²⁷⁹ Angalia hapa. Yeye alisema, “Baba yako na mimi tulikutafuta, usiku na mchana, kwa machozi.” Yeye aliukanusha ushuhuda wake wa kwanza. Alimwita Yusufu baba Yake.

²⁸⁰ Sasa mwangalie Mvulana huyu mwenye umri wa miaka kumi na miwili, akiwa hajui yale aliyosema. Alikuwa ni Mvulana tu, bali alikuwa ni Neno. Unaona? Yeye alisema, “Hamjui kwamba inanipasa kufanya kazi ya Baba Yangu?” Mnaona Neno likisahihisha kosa? Mnaona?

²⁸¹ Yeye mama alikuwa akitoa ushuhuda baada ya Mvulana huyo kulelewa; yote yalikuwa yamekwisha sasa, yeye mama, unaona, “Baba Yako na mimi tumekutafuta,” akienda vile vile hasa... Alisema alikuwa na mimba ya Mtoto huyu kwa uweza wa “Roho Mtakatfu,” halafu akimwita “Yusufu” ndiye baba.

²⁸² Na maskini Mvulana huyu, Mtoto mwenye umri wa miaka kumi na miwili, hana elimu hata kidogo, mbona, bali ni Mvulana tu mwenye umri wa miaka kumi na miwili. Baba hakuwa akiishi ndani Yake wakati huo; kwa maana alikuja kwenye siku aliyombatiza, “Alimwona Roho wa Mungu akishuka, unaona, na akaingia ndani Yake.” Lakini, angalia, maskini Mvulana huyu mwenye umri wa miaka kumi na miwili, akiwa Neno; Yeye alizaliwa Aliyetiwa Mafuta, unaona, apate kutiwa mafuta. Naye ndiye huyu hapa, “Hamjui ya kwamba inanibidi kufanya kazi ya Baba yangu?”

²⁸³ Akasema, “Baba yako pamoja na mimi tumekuwa tukikutafuta.” Kama Yusufu alikuwa ndiye baba Yake, Yeye angalikuwa pamoja naye kwenye biashara yake, akitengeneza milango na kujenga nyumba.

²⁸⁴ Lakini alikuwa yuko hekaluni, akiyanyosha hayo madhehebu. Unaona? “Hamjui ya kwamba yanipasa niwe katika kazi ya Baba Yangu?” Unaona jinsi Neno la Mungu lilivyosahihisha kosa hilo, katika Mtoto huyo! Amina. Mungu awabariki.



KITENDAWILI SWA64-0206B

(Paradox)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza Alhamisi asubuhi, tarehe 6 Februari, 1964, kwenye kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel kwenye Mkahawa wa Salad Bowl huko Bakersfield, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org